



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA
KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI
(PSLE) 2022**

URAIJA NA MAADILI



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA
KUMALIZA ELIMU YA MSINGI
(PSLE) 2022**

06 URAIA NA MAADILI

Kimechapwa na

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023

Haki zote zimehifadhiwa.

Yaliyomo

DIBAJI	iv
1.0 UTANGULIZI	5
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI.....	6
2.1 SEHEMU A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi	6
2.2. SEHEMU B: Maswali na Majibu Mafupi.....	79
3.0 HITIMISHO	100
4.0 MAPENDEKEZO	101

DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa kuhusu ufaulu wa watahiniwa wa somo la Uraia na Maadili katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2022. Taarifa hii ina lengo la kutoa mrejesho wa ufaulu kwa walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu watahiniwa walivyojibu mtihani huu. Mtihani huu uliandaliwa kwa kufuata mtaala wa mwaka 2016 ulioanza kutumika mwaka 2017.

Mtihani wa Uraia na Maadili ni tathmini ya mwisho ya Elimu ya Msingi ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha kiwango cha umahiri kilichofikiwa na wanafunzi kwa miaka saba. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho unaonesha mambo ambayo watahiniwa waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika miaka saba ya Elimu ya Msingi. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika somo hili ulikuwa wa kiwango cha wastani (56.31%). Ufaulu huu ulichangiwa na watahiniwa kuwa na umahiri wa kutosha katika maudhui ya umahiri uliotahiniwa katika somo na hivyo kuweza kuelewa matakwa ya maswali na kuandika majibu sahihi.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umebainisha mambo mbalimbali yaliyosababisha watahiniwa kufanya vibaya au vizuri katika mtihani wao. Uchambuzi unaonesha kuwa mambo yaliyosababisha watahiniwa kufanya vizuri katika mtihani huu ni uwezo wa kuelewa matakwa ya maswali na maudhui ya umahiri uliotahiniwa. Watahiniwa waliofanya vibaya katika mtihani huu hawakuwa na uwezo wa kutambua matakwa ya maswali na pia hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maudhui ya umahiri mbalimbali uliotahiniwa na hivyo kushindwa kuandika majibu sahihi.

Baraza la Mitihani lina imani kuwa taarifa hii itawawezesha viongozi wa elimu, walimu wakuu wa shule, walimu na wadau wengine wa elimu kuchukua hatua madhubuti katika kuborehsa ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza linapenda kuwashukuru maafisa mitihani, wataalamu wa TEHAMA na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kutayarisha taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi katika somo la Uraia na Maadili ulifanyika tarehe 6 Oktoba 2022. Jumla ya watahiniwa 1,384,186 walisajiliwa kufanya mtihani huu. Hata hivyo ni watahiniwa 1,350,793 (97.58%) pekee ndio waliweza kufanya mtihani huu. Aidha ufaulu wa watahiniwa katika somo hili unaonesha kuwa watahiniwa 1,103,632 (81.87%) walifaulu na watahiniwa 247,161 (18.13%) hawakufaulu.

Mtihani ulikuwa na maswali 40 ya kuchagua na maswali 5 ya majibu mafupi ambayo yaligawanyika katika sehemu mbili A na B. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika kila sehemu. Katika swali la 1 hadi 40, watahiniwa walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kisha kuweka kivuli katika herufi hiyo katika fomu maalumu ya OMR. Katika kujibu swali la 41 hadi 45 watahiniwa walielekezwa kuandika majibu yao katika nafasi zilizoachwa wazi kwenye fomu ya kujibia (OMR) kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi. Kila swali katika sehemu A lilikuwa na alama 1, ilihali kila swali katika sehemu B lilikuwa na alama 2 na hivyo kuwa na jumla alama 10.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umegawanya ufaulu wa watahiniwa katika viwango vitatu ambavyo ni vizuri, wastani na hafifu. Ufaulu mzuri unaanza asilimia 60 hadi 100, wastani asilimia 40 hadi 59 na hafifu asilimia 0 hadi 39. Chati za viwango vya ufaulu zimeambatanishwa katika kila swali ili kufafanua ufaulu wa watahiniwa. Viwango vya ufaulu vimeoneshwa kwa rangi tatu tofauti ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano ufaulu wa wastani na rangi nyekundu ufaulu hafifu. Aidha, majibu sahihi yanawakilishwa na alama ya nyota (*) katika majedwali na chati.

Watahiniwa ambao hawakufanya swali au walichagua jibu zaidi ya moja katika swali wamewasilishwa kwenye majedwali na chati kwa kutumia neno “Mengine”. Taarifa hii inawasilisha majibu ya watahiniwa yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu katika somo la Uraia na Maadili. Vilevile, taarifa inabainisha sababu zilizowafanya watahiniwa kuandika jibu sahihi au kipotoshi katika maswali mbalimbali. Inatarajiwa kuwa uchambuzi huu utasaidia

kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili na pia utaboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo.


2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI

2.1 SEHEMU A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi

Swali la 1: Misaada inayotolewa kwa wahitaji ni ya aina mbalimbali kulingana na uhitaji wa watu. Ni kundi lipi **sio** la wahitaji katika jamii?

- A Watoto yatima
- B Wanafunzi wa elimu ya juu
- C Watu wenye ulemavu
- D Wanaoishi katika mazingira hatarishi
- E Waathirika wa majanga

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu makundi ya watu wenye uhitaji katika jamii. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 1,117,123 (82.70%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 233,670 (17.3%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi B, *Wanafunzi wa elimu ya juu* walielewa kuwa kundi hili ni la watu wanaosoma vyuo vya kati au vya juu ili wapate stashahada na shahada mbalimbali. Kundi hili sio lenye uhitaji kwakuwa baadhi yao ni waajiriwa na wengine hupewa mikopo na serikali. Chati Na 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 1: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 57,566 (4.26%) waliochagua kipotoshi A, *Watoto yatima* hawakuwa sahihi kwa kuwa watoto yatima ni kundi la wahitaji kwa sababu ya kukosa wazazi wa kuwalea na kuwapatia mahitaji ya msingi hasa wakiwa wadogo. Halikadharika, watahiniwa 37,873 (2.80%) waliochagua kipotoshi C, *Watu wenge ulemavu* walikosea kwa sababu kundi hili linahusisha watu wenye ulemavu wa mwili au akili au vyote kwa pamoja kama vile maalbino, viziwi, ulemavu wa uneni, ulemavu wa kuona, ulemavu wa akili na usonji. Kundi hili ni la wenye uhitaji kutoka kwa watu wengine, serikali na asasi za kiraia ili kutatua changamoto wanazokumbana nazo katika mazingira yanayowazunguka na katika kutimiza shughuli zao za kila siku kulingana na mili au ulemavu wao.


Aidha, watahiniwa 68,373 (5.06%) waliochagua kipotoshi D, *Wanaoishi katika mazingira hatarishi*, hawakuwa sahihi kwani watu hawa wanaoishi katika mazingira hatarishi wanaweza kuwa katika hatari ya kutumia madawa ya kulevyta, kunyanyaswa kingono, kufanya uhalifu na kupata magonjwa. Hivyo, wanahitaji kusaidiwa ili kuepukana na hali hiyo. Mwisho, watahiniwa 59,862 (4.43%) waliochagua kipotoshi E, *Waathirika wa majanga*, hawakuwa sahihi kwa vile majanga ya asili kama tetemeko la ardhi na mafuriko husababisha madhara makubwa kwa waathirika, kama vile kupoteza mali, kukosa malazi, kupoteza

ndugu na babaiko. Katika hili hii ni wazi kwamba kundi hili huhitaji msaada na uangalizi maalumu.

Swali la 2: Ofisa Mtendaji wa Kata hupatikanaje?

- A Huchaguliwa na madiwani
- B Huchaguliwa na wananchi
- C Huteuliwa na Halmashauri
- D Huajiriwa na serikali
- E Huchaguliwa na wenyeviti wa mitaa

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii*. Katika swalii hili watahiniwa walitakiwa kubaini namna Ofisa Mtendaji wa Kata anavyopatikana. Swali lilijibwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 293,931 (21.76%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 1,056,862 (78.24%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi D, *Huajiriwa na serikali* walikuwa na uelewa kuwa maofisa watendaji wa kata ni watumishi wa umma, ambao wameajiriwa na serikali kwa mikataba ya kudumu na huweza kuhamishwa kutoka Kata moja kwenda nyingine. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 2: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2


Kwa upande mwingine, watahiniwa 252,586 (18.70%) waliochagua kipotoshi A, *Huchaguliwa na madiwani* na

watahiniwa 316,420 (23.42%) waliochagua kipotoshi B, *Huchaguliwa na wananchi*, na hata watahiniwa 360,468 (26.69%) waliochagua kipotoshi C, *Huteuliwa na Halmashauri* hawakuwa sahihi, kwakuwa madiwani pamoja na baraza lao hawana mamlaka ya kuchagua wala kuteua maofisa watendaji wa kata bali wana mamlaka ya kuchagua viongozi wa kisiasa kama vile Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Meya wa Manispaa au Jiji fulani. Aidha, watahiniwa 107,867 (7.99%) waliochagua kipotoshi E, *Huchaguliwa na wenyeviti wa mitaa*, hawakujua kwamba maofisa watendaji wa Kata hawagombe wala kushiriki katika chaguzi za serikali za mitaa ili kupata nafasi hizo. Nafasi zao hutangazwa na Sekretariati ya Ajira katika utumishi wa umma ambacho ni chombo kilichoundwa na sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 na marekebisho yake Na.18 ya mwaka 2007 kifungu cha 29(1).

Swali la 3: Ni kipi kati ya vifuatavyo **hakiwezi** kuitambulisha shule?

- A Madarasa ya shule B Mipaka ya shule
- C Kaulimbiu ya shule D Nembo ya shule
- E Wimbo wa shule

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima jambo au kitu ambacho hakiwezi kuitambulisha shule fulani. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 592,023 (43.83%) walijibu swalii hili kwa usahihi na watahiniwa 758,770 (56.17%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Madarasa ya shule*, walijua kuwa madarasa ni vyumba ambavyo hutumiwa katika mchakato wa kufundisha na kujifunza. Hivyo madarasa hayawezi kuwa ni alama inayoweza kuitambulisha shule. Kiuhalsia alama za shule zinatakiwa kuwa za kipekee ili kuweza kutofautisha shule moja na nyingine. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 3: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3


Kwa upande mwingine, watahiniwa 525,476 (38.90%) waliochagua kipotoshi B, *Mipaka ya shule*, hawakuwa sahihi kwa kuwa mipaka huonesha kwa usahihi eneo la shule na mahali ambapo ni kikomo na eneo lingine. Kwa mantiki hiyo, mipaka inaweza kutumika kuitambulisha shule fulani. Zaidi ya hapo watahiniwa 113,646 (8.41%) waliochagua kipotoshi C, *Kaulimbiu ya shule*, hawakuwa sahihi kwa kuwa kauli mbiu ni sentensi au usemi wenye kubeba malengo na Imani ya shule fulani. Hivyo, ni mionganini mwa vitu vinavyoitambulisha shule, na watahiniwa 57,847 (4.28%) waliochagua kipotoshi D, *Nembo ya shule* hawakuwa sahihi kwasababu ni mchoro uliobuniwa kutumika kama utambulisho au alama ya shule fulani, hivyo inaitambulisha shule.

Mwisho, watahiniwa 44,922 (3.33%) waliochagua kipotoshi E, *Wimbo wa shule* hawakuwa sahihi kwasababu ni wimbo unaotungwa maalumu kwa ajili ya shule fulani na huimbwa na wanafunzi wa shule husika mara kadhaa au kwenye matukio maalumu ili kuisifu na kuienzi shule yao, hivyo kuwa tofauti na shule nyingine. Kwa ujumla; kaulimbiu ya shule, nembo ya shule, mipaka ya shule pamoja na wimbo wa shule haviko sawa kwa shule zote kwasababu vimekusudiwa kuitambulisha shule fulani.

Swali la 4: Mwanafunzi mwenye tabia nzuri ni lazima awe mwenye kujipenda. Nini maana ya kujipenda?

- A Kujisifia mara zote
- B Kuwakubali wengine
- C Kustahimili na kujikubali
- D Kujitegemea katika masomo
- E Kujithamini na kujikubali

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii* na lililenga kupima uwezo wa watahiniwa juu ya uelewa wa dhana ya kujipenda. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 936,810 (69.35%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 413,983 (30.65%) hawakujuhu kwa usahihi. Watahiniwa waliobaini jibu sahihi E, *Kujithamini na kujikubali* walijua kuwa kujithamini hutokea wakati mtu anapojonja wa thamani. Pia, kujikubali ni kitendo au hali ya kutambua utu wako na tabia bainishi zikiwa hasi au chanya na kuzikubali. Hii inahusisha mtazamo wa kimaumbile na kiakili. Kujipenda kuna sifa za kujitunza kiafya, kuepuka matendo mabaya sambamba na kuwa na tabia njema. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 4: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4

Kwa upande mwingine, watahiniwa 84,510(6.26 %) waliochagua kipotoshi A, *Kujisifia mara zote* hawakuwa sahihi kwani kujisifia

mara zote ni kitendo au hali ya kujitukuza au kujikweza kuliko uhalisia ulivyo. Hii inadhihirisha kiburi au ubinafsi wa mtu. Vilevile, watahiniwa 84, 338 (6.24%) waliochagua kipotoshi B, *Kuwakubali wengine* hawakuwa sahihi kwakuwa kuwakubali wengine ni uwezo wa kuona kuwa wengine wana haki ya kuwa wa kipekee kama walivyo.

Vilevile, watahiniwa wengine 141,820 (10.50%) walichagua kipotoshi C, *Kustahimili na kujikubali*. Watahiniwa hao hawakuwa sahihi kwani kujikubali ni mojawapo ya ishara au tendo la kuonesha kujipenda ilihali kustahimili humaanisha mchakato wa matokeo ya kuvumilia au kuchukuliana/kukabiliana na changamoto au mazingira magumu katika maisha kiakili, kihisia na kitabia kisha kijiweka sawa kwa kuzingatia mahitaji ya ndani na nje yake. Hii ni hali ya kuchukuliana na hali mpya (changamoto) kisha kurejea katika hali ya kwaida au ya awali.


Aidha, watahiniwa wengine 88,876 (6.58%) waliochagua kipotoshi D, *Kujitegemea katika masomo* hawakuwa sahihi kwa sababu kujitegemea katika masomo ni kitendo cha kutumia akili yake mwenyewe na kutokushawishiwa au kuongozwa kwa namna yoyote ile na watu wengine, matukio au vitu vingine katika taaluma au ujifunzaji.

Swali la 5: Ni kitendo gani kati ya hivi vifuatavyo kinaweza kutumika katika kutokomeza ukandamizaji wa kijinsia katika jamii?

- A Kutoa elimu kwa wote
- B Kutoa elimu kwa wanaume
- C Kutoa elimu kwa watu wazima
- D Kutoa elimu kwa watoto
- E Kutoa elimu kwa vijana

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii* na liliwataka watahiniwa wabainishe matendo yanayoonesha usawa wa kijinsia katika jamii. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 1,011,149 (74.86%) walijibu swali hili kwa

usahihi na watahiniwa 339,644 (25.14%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kutoa elimu kwa wote* walielewa kuhusu dhana ya ukandamizaji wa kijinsia kuwa ni hali ya jinsi moja kutendea au kuchukulia jinsi nyingine tofauti hasa katika namna mbaya au isiyokubalika katika kutekeleza majukumu yao katika jamii Kinyume na jinsi nyingine inavyotendewa. Pia, watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa, jamii huhusisha watu wote waishio katika eneo fulani na jamii inatakiwa kujua juu ya matokeo hasi ya unyanyasaji wa kijinsia. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




Chati Na. 5: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5

Kwa upande mwingine, watahiniwa 119, 958 (8.88%) waliochagua kipotoshi B, *Kutoa elimu kwa wanaume*, 76,820 (5.69%) waliochagua kipotoshi C, *Kutoa elimu kwa watu wazima*, 70,953 (5.25%) waliochagua kipotoshi D *Kutoa elimu kwa watoto* na 59,045 (4.37%) waliochagua kipotoshi E, *Kutoa elimu kwa vijana*, hawakuwa sahihi kwa sababu utoaji wa elimu au maarifa kwa lengo la kutokomeza ukandamizaji wa kijinsia katika jamii unahusisha wanajamii wote na sio sehemu tu ya wanajamii kama vile wanaume, vijana, watoto au watu wazima. Katika hili, utoaji wa elimu ili kutokomeza ukandamizaji wa kijinsia kwa kundi moja tu la wanajamii humaanisha kutengwa au kutohusishwa au kutoshirikishwa kwa makundi mengine, hivyo kuendeleza tabia hiyo isiyofaa katika jamii.

Swali la 6: Jambo lipi **sio** huduma inayoweza kutolewa kwa watu wenye ulemavu?

- | | |
|----------------------|--------------------|
| A Ushauri | B Uadilifu |
| C Makazi | D Msaada wa kiafya |
| E Msaada wa kisheria | |

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubainisha huduma isiyotolewa kwa watu wenye mahitaji maalumu katika jamii. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 577,963 (42.79%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 772,830 (57.21%) hawakujibu kwa usahihi. Jibu sahihi lilikuwa B, *Uadilifu*. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi wallikuwa na uelewa wa kutosha juu ya watu wenye ulemavu kuwa ni watu waliopungukiwa moja kati ya uwezo wa kiakili, kimwili au kimaumbile tofauti na wengine. Pia, watahiniwa hao walitambua huduma mahususi zitolewazo kwa watu wenye ulemavu kuwa ushauri, msaada wa kiafya, kisheria na makazi. Aidha, watahiniwa hao waliweza kutambua kuwa uadilifu ni hali ya kutenda haki, kuwa mwaminifu na kusimamia kanuni zilizowekwa ili kutimiza ahadi na kufichua maovu. Hivyo, uadilifu sio mojawapo ya huduma mahususi zitolewazo kwa watu wenye ulemavu na kwamba uadilifu ni sehemu ya maadili mema. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 6: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6

Hata hivyo, watahiniwa 118,977 (8.81%) waliochagua kipotoshi A, *Ushauri* hawakuwa sahihi kwa kuwa ushauri ni maoni au nasaha atoayo mtu kwa mtu mwingine kwa habari ya nini afanye au awe na mwitikio gani juu ya hali fulani anayopitia. Huduma hii inahitajika sana kwa watu wenyewe ulemavu ili kupata ufumbuzi wa haraka na unaostahili juu ya changamoto wanazopitia na hatimaye kufikia mategemeo yao. Matarajio yao yanaweza kuhusiana na maswala ya kielimu, ajira au biashara. Watahiniwa 341,410 (25.27%) kadhalika walichagua kipotoshi C, *Makazi*. Hao pia hawakuwa sahihi kwa sababu makazi ni mahali au makao aishipo mtu. Watu wenyewe ulemavu wanapaswa kupatiwa huduma hii ya makazi kwa ajili ya usalama wao dhidi ya hatari mbalimbali na pia kujikinga na hali mbaya ya hewa.

Vilevile, watahiniwa 74,398 (5.51%) waliochagua kipotoshi D, *Msaada wa kiafya* hawakuwa sahihi kwani msaada wa kiafya ni huduma zote zinazotolewa kwa ajili ya kuboresha ustawi wa mwili au akili ya mtu. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa watu wenyewe ulemavu wanahitaji kupatiwa huduma ya uangalizi wa hali zao kiafya ili kujikinga na magonjwa mbalimbali na kupata matibabu ya magonjwa wanayopata. Pia, watu wenyewe ulemavu huhitaji vifaa tiba kama vile magongo ya kutembelea na elimu ya afya. Watahiniwa 221,360 (16.39%)


waliochagua kipotoshi E, *Msaada wa kisheria* pia, hawakuwa sahihi kwa sababu msaada wa kisheria ni ushauri kuhusu mambo yanayohusiana na sheria hasa pale zinapojitokeza changamoto za kisheria. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa watu wenyewe ulemavu wanahitaji huduma hiyo kwani hukumbwa na changamoto mbalimbali katika maisha yao ya kila siku hivyo kuhitaji msaada wa kisheria. Changamoto hizo zinaweza kuwa kudhuriwa kimwili, kunyang'anywa mali na ukatili wa kingono.

Swali la 7: Ni madhara gani hutokea kutokana na ukandamizwaji wa wanawake katika jamii?

- A Kuongezeka kwa vifo katika jamii
- B Kujengeka kwa matabaka katika jamii
- C Kuongezeka kwa ufahamu wa haki za binadamu
- D Kuongezeka kwa ndoa halali katika jamii
- E Kuongezeka kwa asasi za kiraia

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuithamini Jamii* na lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu masuala ya unyanyasaji wa kijinsia katika jamii hususan masuala yanayohusiana na wanawake na madhara yake katika jamii. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 247,717 (18.34%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 1,103,076 (81.66%) hawakujibu kwa usahihi. Jibu sahihi lilikuwa B; *Kujengeka kwa matabaka katka jamii*. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa mambo yanayohusu madhara ya unyanyasaji wa wanawake katika jamii kuwa ni kama kuigawa jamii katika matabaka ya kijinsi; hali inayo waathiri zaidi wanawake kuliko wanaume. Matabaka haya huondoa usawa katika upataji wa elemu, kumiliki rasilimali muhimu kama ardhi na pia huwanyima nafasi ya kushiriki kufanya maamuzi katika ngazi mbalimbali. Madhara mengine yatokanayo na ukandamizwaji wa wanawake katika jamii ni pamoja na kundelea kuwepo kwa vitendo vya ukatili dhidi ya

wanawake, kuongezeka kwa umaskini na ujinga na kukithiri kwa migogoro katika jamii. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 7: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7

Kwa upande mwingine, watahiniwa 761,064 (56,34%) waliochagua kipotoshi A; *Kuongezeka kwa vifo katika jamii* hawakuwa sahihi kwa sababu kuongezeka kwa vifo si madhara ya moja kwa moja yanayotokana na ukandamizwaji wa kijinsia bali ni matokeo yanayoweza kusababishwa na matukio au mambo anuwai katika jamii kama vile magonjwa, na ajali. Vilevile watahiniwa 104,008 (7.70%) waliochagua kipotoshi C; *Kuongezeka kwa ufahamu wa haki za binadamu* nao hawakuwa sahihi kwani kuongezeka kwa ufahamu wa haki za binadamu ni matokeo ya mchakato wa kimkakati wa kuwafanya watu kuelewa, kuheshimu na kulinda stahiki zao kama binadamu katika jamii. Pia, watahiniwa 104,684 (7.75%) waliochagua kipotoshi D; *Kuongezeka kwa ndoa halali katika jamii* hawakuwa sahihi kwa sababu kuongezeka kwa ndoa halali ni kiashiria cha jamii kuwapa nafasi wanawake/wanaume kuwa na ufahamu juu wa mahusiano ili kuepukana na migogoro isiyo ya lazima katika ndoa kinyume na ndoa za lazima au utotoni katika jamii.


Aidha, watahiniwa 115, 358 (8.54%) waliochagua kipotoshi E; *Kuongezeka kwa asasi za kiraia*, hawakuweza kutofautisha kati ya madhara yatokanayo na ukandamizwaji wa wanawake na

matokeo ya mageuzi ya kijamii na kisiasa. Hawakuweza kung'amua kwamba mageuzi ya kijamii na kisiasa yalipelekea kuongezeka kwa asasi za kiraia ambazo kimsingi hulinda na kutetea maslahi ya makundi maalumu. Kuongezeka kwa asasi hizi kumesaidia kuongeza ufahamu wa wanawake katika kutambua haki zao, hivyo kuwawezesha kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi, na hivyo kuleta usawa wa kijinsia katika jamii.

Swali la 8: Kila raia wa Tanzania ana wajibu wa kulinda amani ya nchi. Ni kwa vipi utatimiza wajibu huu ?

- A Kwa kutii sheria za nchi
- B Kwa kutii maelekezo ya wataalamu
- C Kwa kutoa taarifa kwa wafadhili
- D Kwa kutoa elimu kwa wazee
- E Kwa kutenda haki kwa watu wachache

Swali lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu njia ambazo raia anaweza kuzitumia kutimiza wajibu wa kulinda amani ya nchi. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 1,144,950 (84.76%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 205,843 (15.24%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A; *Kwa kutii sheria za nchi*, walifahamu kwamba kila raia ana wajibu wa kufuata na kutii kanuni na taratibu ambazo nchi imejiwekea ili kudhibiti mienendo na mahusiano ya watu katika nchi. Kwa kufuata taratibu hizo raia hutimiza wajibu wake wa kulinda amani ya nchi kwani huepusha migongano isiyo ya lazima ambayo ingeweza kuiweka rehani amani ya nchi. Pia, raia hulinda amani ya nchi kwa kuwapenda watu wengine na kuheshimu tamaduni za maisha yao, kutoshiriki katika vitendo vya uhalifu na kutoa taarifa kuhusu tukio au kitendo chochote kinachohatarisha usalama wa nchi. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




Chati Na. 8: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa 49,108 (3.64%) walichagua kipotoshi B; *Kwa kutii maelekezo ya wataalamu* na watahiniwa 61,404 (4.55%) walichagua kipotoshi C; *Kwa kutoa taarifa kwa wafadhili*. Watahiniwa hao hawakuwa sahihi kwa sababu ni kitendo cha kufuata miongozo ya kitaalamu katika ufanyaji au utekelezaji wa shughuli fulani. Wakati huohuo kutoa taarifa kwa wafadhili humaanisha mfumo maalum wa upenanaji wa mrejesho kati ya watu, nchi au mashirika hisani. Hivyo basi, vipotoshi vyote viwili haviakisi namna ambayo raia anaweza kuitumia kutimiza wajibu wake wa kulinda amani ya nchi. Vilevile, kipotoshi D; *Kwa kutoa elimu kwa wazee*; ambacho kilichachaguliwa na watahiniwa 40,083 (2.97%) hakikuwa sahihi kwa sababu kilihusu mchakato wa kuwajengea uelewa watu wenyewe umri mkubwa juu ya mambo mbalimbali. Utoaji wa elimu kwa wazee ni wajibu wa serikali na asasi zingine za kiraia. Pia, watahiniwa 44,918 (3.33%) waliochagua kipotoshi E; *Kwa kutenda haki kwa watu wachache* hawakuwa sahihi kwa sababu kufanya hivyo huondoa usawa wa watu katika nchi kwani huruhusu watu wachache kufaidika na utoaji haki wakati walio wengi wakitaabika kutokana na kutotendewa haki. Kitendo hiki huweza kuharibu zaidi amani ya nchi kuliko kuilinda na kinaweza kujenga matabaka na migogoro katika jamii.

Swali la 9 : Katika jamii iliyostaarabika watu hujiheshimu na hujikinga na mambo yanayowaletea madhara. Je, kitendo hicho huitwaje?

- | | | | |
|---|------------|---|-------------------|
| A | Kujijali | B | Kuwajali wengine |
| C | Kujipenda | D | Kuwapenda wengine |
| E | Kujihamini | | |

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuithamini Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubainisha vitendo vyta kujijali na kuwajali wengine dhidi ya mambo yanayoweza kuwalettea madhara. Swali lilijibwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 748,809 (55.43%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 601,987 (44.57%) hawakujibu kwa usahihi. Jibu sahihi lilikuwa A; *kujijali*. Watahiniwa waliochagua jibu hili walifahamu kuwa kujijali kunahusisha kutambua matendo yanayoweza kukuletea madhara au kuzingatia jambo lenye manufaa katika maisha yako. Baadhi ya matendo hayo ni kama; kujifunika mwamvuli wakati mvua inanyesha, kupiga mswaki kila baada ya kula chakula, kuoga na kuvalaa sweta wakati wa baridi kali, kuwa nadhifu, kunawa mikono baada ya kutoka chooni, kuvalaa viatu na kutochezea maji machafu. Chati Na. 9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 9: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9


Watahiniwa wengine 135,754 (10.05%) walichagua kipotoshi B; *Kujajali wengine* na watahiniwa 252,293 (18.68%) walichagua kipotoshi C; *Kujipenda*. Majibu hayo sio sahihi kwa kuwa kuwajali wengine kunamaanisha kutenda mambo mema kwa wengine kwa namna ambayo wewe ungependa kutendewa. Baadhi ya matendo ya kuwajali wengine ni kama; kuwapenda, kuwaheshimu, kuwasaidia na kuwakinga na mambo yatakayowaletea madhara. Hivyo matendo hayo yote hayajumuishi nafsi ya kwanza inayohusiana na kujijali. Pia, kujipenda ni kujithamini na kujikubali ambapo pia ni tofauti na takwa la kujijali. Watahiniwa 86,988 (6.44%) walichagua kipotoshi D; *Kuwapenda wengine*. Watahiniwa hao hawakutam bua kuwa walikosea kwa sababu kuwapenda wengine ni kuonesha hali ya mguso wa moyo kwa watu wengine. Kwa mfano, mwanafunzi anayewapenda wenzake atawasalimia, atawasaidia kuwapa ushauri mbalimbali. Mwisho, Watahiniwa 110,472 (8.18%) waliochagua kipotoshi E; *Kujiamini*, hawakujuwa kuwas kuwa kujiamini humaanisha kuwa na imani juu ya uwezo na sifa zako binafsi. Hii humfanya mtu kujikubali na kuweza kujiwekea matarajio na malengo katika maisha, kusimamia anachokiamini na kuhimili hoja kinzani.

Swali la 10: Mahusiano mabaya baina ya wanajamii huleta athari gani?

- A Vurugu na upendo B Chuki na upendo
- C Umaskini na ujinga D Migogoro na mapigano
- E Umbea na umaskini

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuithamini Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa katika kubainisha matokeo ya mahusiano mabaya katika jamii. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 1,042,767 (77.20%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 308,026 (22.80%) walikosea. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi D, *Migogoro na mapigano* walielewa kwamba mahusiano mabaya husababisha mifarakano

na chuki na isipopatiwa suluhu katika hatua za awali basi huleta migogoro, machafuko na uhasama. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 10: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10

Kwa upande mwingine, watahiniwa 50,484 (3.74%) waliochagua kipotoshi A, *Vurugu na upendo* na watahiniwa 61,537(4.56%) waliochagua kipotoshi B, *Chuki na upendo* walihusisha dhana hizo na upendo wakati upendo hauwezi kuwa matokeo ya mahusiano mabaya kwa namna yoyote. Upendo hufanya watu kuwakubali wengine, kuvumiliana katika mapungufu yao, kuheshimiana na kusaidiana katika shida na raha; na hizi ndizo tabia za mahusiano mazuri katika jamii.


Aidha, watahiniwa 125,779 (9.31) waliochagua kipotoshi C, *Umaskini na ujinga* pamoja na watahiniwa 57,209 (4.24%) waliochagua kipotoshi E, *Umbea na umaskini* hawakutambua kuwa umasikini ni hali ya mtu au jamii kushindwa kumudu mahitaji au huduma za msingi na muhimu. Umaskini ukikithiri huleta ufukara na ukata. Aidha, umasikini husabishwa na mambo mbalimbali kama; uvivu, ukosefu wa ajira na teknolojia duni. Halikadhalika, ujinga ni hali ya kutokujua kitu fulani mfano kusoma na kuandika ambavyo husabishwa na kukosa elimu msingi. Mwisho, umbea ni tabia ya udaku yenye maana ya kupekua mambo ya mtu na kuyaeneza kwa lengo la kuchonganisha. Tabia hii husababisha mahusiano mabaya na

migogoro katika jamii. Pia, ni suala ambalo halina mahusiano na takwa la swali.

Swali la 11: Ni njia ipi bora zaidi ya kufikisha taarifa au maoni kwa uongozi wa shule kuhusu vitendo visivyofaa shuleni?

- A Kutumia sanduku la maoni
- B Kutumia mukutano wa wazazi
- C Kutumia wazazi ili kutoa malalamiko
- D Kutumia ubao wa matangazo
- E Kutumia Sanduku la Posta

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu njia sahihi zinazoweza kutumiwa ili kufikisha taarifa katika uongozi wa shule. Swali lilijibowiwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 758,334 (56.14%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 592,459 (43.86%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kutumia sanduku la maoni* walifahamu kuwa masanduku ya maoni yametengenezwa kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa urahisi na humuhakikishia faragha mtoe maoni au ushauri shuleni. Pia, haina gharama na ni nzuri kwa wanafunzi na walimu kwa ujumla. Chati Na. 11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 11: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11

Hata hivyo, kuna baadhi ya watahiniwa ambao hawakuchagua jibu sahihi. Kwa mfano; watahiniwa 215,323 (15.94%) waliochagua kipotoshi B, *Kutumia mkutano wa wazazi* na watahiniwa 103,816 (7.69%) waliochagua kipotoshi C, *Kutumia wazazi ili kutoa malalamiko* hawakuelewa kuwa wazazi wanakuwa nyumbani hivyo siyo rahisi kujua mambo ya shulenii na changamoto zake kwa kulinganisha na wanafunzi wa shule husika. Pia, njia zote mbili zinaweza kusababisha mifarakano baina ya wanafunzi, wazazi na uongozi wa shule hasa pale maoni au taarifa zinazotolewa kwa uwazi huwa zinakarahisha.


Vilevile, watahiniwa 94,642 (7.01%) waliochagua kipotoshi D, *Kutumia ubao wa matangazo* hawakuwa sahihi kwa kuwa ubao wa matangazo hutumika kutoa taarifa za wazi kama; matokeo ya wanafunzi, ratiba na masuala ya kitaaluma. Vilevile, ubao wa matangazo hauwezi kutoa mambo muhimu ya siri. Mwisho, watahiniwa 162,019 (11.99%) waliochagua kipotoshi E, *Kutumia Sanduku la Posta* nao hawakuwa sahihi kwa sababu sanduku la posta ni maalumu kwa ajili ya kupokea barua na nyaraka mbalimbali za shule na za jamii. Zaidi, njia ya Sanduku la Posta inachukua muda mrefu na ni gharama hivyo, si rafiki kutumiwa na mwanafunzi katika kutoa taarifa kuhusu vitendo visivyofaa shulenii.

Swali la 12: Mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi Mapinduzi ameanzisha kitengo cha ushauri nasaha katika shule yake. Kitengo hicho kina umuhimu gani?

- A Kutoa mwongozo wa kutatua changamoto
- B Kueleza mipango ya shule kwa undani
- C Kudhibiti nidhamu za wanafunzi
- D Kuandaa mipango ya usafi shulenii
- E Kuandaa orodha ya wanafunzi wahitaji

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuithamini Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa wa kutathmini faida za kitengo cha ushauri nasaha shulenii. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793

ambapo watahiniwa 991,162 (73.38%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 359,631(26.62%) walikosea. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kutoa mwongozo wa kutatua changamoto* walijua kuwa unasihi hutoa mwongozo wa namna ya kutatua tatizo la mtu au kikundi cha watu katika jamii. Pia, watahiniwa walijua kuwa huduma ya unasihi huwawezesha watu kujitambua na kujiongoza, huwajengea uwezo wa kujitambua katika kukua kwao, huwfanya watu wajirekebishe kimwenendo ili wakubalike katika jamii na mwisho huwawezesha watu kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimaisha. Chati Na. 12 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Chati Na. 12: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12*


Kwa upande mwingine, watahiniwa 94,259 (6.98%) waliochagua kipotoshi B, *Kueleza mipango ya shule kwa undani* hawakutambua kuwa mipango ya shule inaweza kuelezwa na kamati ya shule wakati wa kuendesha vikao vya wazazi. Kamati ina wajibu wa kuandaa na kuidhinisha mipango ya maendeleo ya shule na mikakati ya utekelezaji wake. Halikadhalika, watahiniwa 121,061 (8.96%) waliochagua kipotoshi C, *Kudhibiti nidhamu za wanafunzi* hawakujua kuwa hilo ni jukumu la mwalimu wa nidhamu ambaye husimamia utii, heshima na maadili ya wanafunzi wote na kuhakikisha kuwa wanafuata sheria na kanuni za shule.

Vilevile, watahiniwa 56,862 (4.21%) waliochagua kipotoshi D, *Kuandaa mipango ya usafi shulen* i hawakuwa sahihi kwa sababu huo ni wajibu wa mwalimu mkuuu msaidizi akishirikiana na walimu wa zamu na viranja wa shule. Mwisho, watahiniwa 72, 884 (5.40%) waliochagua E, *Kuandaa orodha ya wanafunzi wahitaji* hawakutambua kuwa mwenye jukumu hili ni uongozi wa shule ambao pamoja na majukumu mengine unasimamia ustawi wa wanafunzi shulen pamoja na wenyе mahitaji maalumu.

Swali la 13: Ni kitendo gani **hakihusiki** katika kuchafua vyanzo vyatya maji?

- A Kuoga mtoni
- B Kufua nguo mtoni
- C Kukojoa pembezoni mwa mto
- D Kulima kandokando ya mto
- E Kutumia njia salama za uvuvi

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuithamini Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa kutambua kitendo ambacho hakihusiki katika kuchafua vyanzo vyatya maji. Swali lilijibwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 977,223 (72.34%) walijibu swali hili kwa usahihi na 373,570 (22.65%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliobaini jibu sahihi E, *Kutumia njia salama za uvuvi* walielewa kuwa njia salama za uvuvi ni kitendo cha kuvua samaki baharini, mtoni, ziwani au bwawani kwa kutimia njia sahihi kama; ndoana au nyavu zenyе matundu mapana kwa namna iliyo salama kwa mazingira, hivyo kuepuka uchafuzi wa vyanzo vyatya maji. Vilevile, watahiniwa hao walikua na uelewa juu ya vitendo vingine ambavyo huchafua vyanzo vyatya maji kama; kuoga mtoni, kukojoa pembezoni mwa mto, kufua nguo mtoni na kulima kandokando ya mto. Chati Na. 13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 13: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 13*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 71,389 (5.28%) waliochagua kipotoshi A, *Kuoga mtoni* hawakutambua kuwa kuoga mtoni huongeza vitu visiviyotakiwa katika mto. Kwa sababu ya shughuli za binadamu kama; kuoga na kulisha mifugo kwenye kingo za mito. Pia, watahiniwa 52,838 (3.91%) waliochagua kipotoshi B, *Kufua nguo mtoni* hawakuwa sahihi kwani kufua nguo mtoni ni kitendo kinachohusisha matumizi ya sabuni mbalimbali zenyekemikali ambazo baadhi yake zina sumu zinazoweza kuhatarisha maisha ya viumbe hai kwenye maji pamoja na binadamu.


Zaidi, watahiniwa 99,178 (7.34%) waliochagua kipotoshi C, *Kukojoa pembezoni mwa mto* hawakuwa na uelewa wa kutosha kwa kuwa kukojoa pembezoni mwa mto ni kitendo cha kutoa taka mwili kwa njia ya haja ndogo karibu na maji yanayotiririka. Kitendo hiki husababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji, hali inayoweza kuchangia kusambaa kwa magonjwa yanayosambazwa kwa njia ya maji kama; kichochi, kipindupindu, homa ya matumbo na mengineyo. Vilevile, watahiniwa 127, 533 (9.44%) waliochagua kipotoshi D, *Kulima kandokando ya mto* walikosa uelewa wa kutosha kwa kuwa kulima kandokando ya mto ni kitendo cha kuandaa shamba kwa kutifua udongo, hivyo kusababisha mmomonyoko wa udongo kuelekea kwenye chanzo cha maji. Udongo uliotifuliwa ni rahisi kumomonyoka. Pia, shughuli za kilimo kandokando ya

mto husababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji kwani mara nyingi huambatana na matumizi ya kemikali na madawa mbalimbali ya kuulia wadudu na magugu wakati wa kulima.

Swali la 14: Kuna umuhimu gani wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana?

- A Huwasaidia kuhimili mihemko ya miili yao
- B Huwasaidia kujiepusha na magonjwa ya mlipuko
- C Huwasaidia kuhimili ndoa za ukubwani
- D Huwasaidia kujenga ari ya kuwapenda wengine
- E Huwasaidia kufanya maamuzi kwa wachumba watarajiwa

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuithamini Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa kutathmini umuhimu wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 693,946 (51.37%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 656,847 (48.635) hawakujibu kwa usahihi. Waliochagua jibu sahihi A, *Kuwasaidia kuhimili mihemko ya miili yao* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu afya ya uzazi kuwa hutoa ufahamu juu ya hali ya ustawi wa mwili, akili na mahusiano katika jamii na mambo yote yanayohusu mfumo wa uzazi kwa wanawake na wanaume. Katika uhalsia elimu ya afya ya uzazi pamoja na mambo mengine inahusisha ngono salama, njia za uzazi wa mpango, magonjwa ya zinaa, uzazi na ujauzito. Chati Na.14 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 14: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14

Kwa upande mwingine, watahiniwa 358,486 (26.54%) waliochagua kipotoshi B, *Kuwasaidia kujiepusha na magonjwa ya mlipuko* hawakuja kuwa magonjwa ya mlipuko ni magonjwa ambayo huathiri idadi kubwa ya watu katika muda/wakati fulani na wakati mwingine hutokea bila kutegemea. Watahiniwa hao hawakuja kuwa magonjwa ya mlipuko siyo sehemu ya elimu ya afya ya uzazi. Vilevile, watahiniwa 112,087 (8.30%) waliochagua kipotoshi C, *Huwasaidia kuhimili ndoa za ukubwani* hawakuwa sahihi kwa sababu kuhimili ndoa za ukubwani ni kustahimili na pia kutatua changamoto mbalimbali baina ya wanandoa wenye umri wa utu uzima. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa elimu ya afya ya uzazi ni ya muhimu na manufaa kwa vijana kwani inalenga kuwajengea uelewa juu ya mabadiliko ya mwili, kuepusha mimba za utotoni, kuelewa mambo muhimu katika makuzi na kuchochea kuishi kwa kuzingatia maadili.


Aidha, watahiniwa 76,615 (5.67%) waliochagua kipotoshi D, *Huwasaidia kujenga ari ya kuwapenda wengine* hawakuwa sahihi kwa kuwa ari ya kuwapenda wengine ni hali ya kupata hisia za kupenda mtu kutokana na kuvutiwa na uzuri wake au namna alivyo. Kwa ujumla, jambo hilo halihusiani kwa namna yoyote na elimu ya afya ya uzazi. Pia, watahiniwa 91,777 (6.79%) waliochagua kipotoshi E, *Huwasaidia kufanya maamuzi kwa wachumba watarajiwa*, hawakuwa sahihi. Watahiniwa hao

hawakuelewa kuwa kufanya maamuzi kwa wachumba watarajiwa ni kuchagua kwa kuzingatia vigezo ambavyo mtu anakuwa navyo juu ya mtu wa kuishi naye kama mke au mume. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana hulenga kuwalinda vijana dhidi ya hatari zinazoweza kujitokeza dhidi ya afya ya uzazi na kuhimili mihemko ya miili yao.

Swali la 15: Riziki alielezwa umuhimu wa kushirikiana na wengine katika kutekeleza majukumu yake ya nyumbani na shulen. Ni mambo yapi kati ya yafuatayo ni majukumu ya nyumbani?

- A Kufagia, kucheza na kumwagilia bustani
- B Kumwagilia bustani, kudeki na kuwa kiongozi
- C Kufagia, kudeki na kumwagilia bustani
- D Kupiga kura, kufagia na kudeki
- E Kudeki, kusafisha zahanati ya kijiji na kufagia

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini na kutofautisha majukumu ya nyumbani na ya shulen. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 na uchambuzi unaonesha kuwa mionganii mwao watahiniwa 927,698 (68.68%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 423,095 (31.32%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi C, *Kufagia, kudeki na kumwagilia bustani*, walielewa kuhusu majukumu hayo ambayo ni pamoja na kuwasaidia wazazi wao kwa kufanya kazi ndogo ndogo kama kumwagilia bustani, kufagia na kupiga deki ili waweze kuwa watu wanaowajibika wakiwa wakubwa. Chati Na. 15 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Chati Na. 15: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 15

Kwa upande mwingine, watahiniwa 202,332 (14.98%) waliochagua kipotoshi A, *Kufagia, kucheza na kumwagilia bustani* hawakuwa sahihi kwa sababu kichaguzi hicho kilihusisha tendo la kucheza ambalo kimsingi ni burudani na sio kazi, hivyo haliwezi kuwa kati ya majukumu ya nyumbani ingawa kufagia na kumwagilia bustani ni majukumu ya nyumbani. Vilevile, watahiniwa 65,245 (4.83%) waliochagua kipotoshi B, *Kumwagilia bustani, kudeki na kuwa kiongozi* hawakuwa sahihi kwani kipotoshi hiki kilihusisha neno kuwa kiongozi ambalo humaanisha kutoa njia/muongozo/maelekezo kwa wengine au kuwa mkuu au msimamizi wa kazi au shughuli fulani. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa katika ngazi ya familia viongozi ni baba na mama, watoto hawatarajiwi kuwa viongozi katika ngazi hiyo.


Pia, watahiniwa 65,069 (4.82%) waliochagua kipotoshi D, *Kupiga kura, kufagia na kudeki* hawakuwa sahihi kwa sababu kipotoshi hiki kilihusisha kupiga kura ambalo ni zoezi la kuchagua viongozi katika ngazi fulani. Watahiniwa hao walikosa maarifa kubaini kuwa kupiga kura siyo jukumu la nyumbani isipokuwa la shulenii au kwenye jamii. Aidha, watahiniwa 79,340 (5.87%) waliochagua kipotoshi E, *Kudeki, kusafisha zahanati ya kijiji na kufagia* hawakuwa sahihi kwani kusafisha zahanati ya kijiji, ni jukumu linaloweza kutekelezwa na jamii nzima hususan

watu wazima. Hivyo kusafisha zahanati ya kijiji ni wajibu wa jumuiya ya kijiji husika.

Swali la 16: Barabara, majengo ya shule na zahanati ni miundombinu ya jamii katika kijiji. Nani ana jukumu la kuilinda?

- A Kamati ya maendeleo ya kijiji
- B Afisa maendeleo wa kijiji
- C Wanakijiji wote
- D Jeshi la polisi
- E Walimu na wazazi

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uelewa wa mtahiniwa juu ya mtu/watu wenyewe wajibu wa kulinda miundombinu ya kijijini. Swali lilitjibowi na watahiniwa 1,350,793. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 984,429 (72.88%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 366,364 (27.12%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa wenyewe maarifa ya kutosha walichagua jibu sahihi C, *Wanakijiji wote* na walitambua kuwa jukumu la kulinda miundombinu ya jamii linahitaji nguvu ya pamoja, hivyo basi, kila mwanajamii anatakiwa kushiriki kuilinda miundombinu hiyo kwa ajili ya matumizi endelevu ya wanajamii. Chati Na. 16 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 16: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 16.

Watahiniwa wengine 117,741 (8.72%) waliochagua kipotoshi A, *Kamati ya maendeleo ya kijiji* hawakuwa sahihi kwa kuwa kamati hiyo huwajibika kubuni, kupanga, kuanzisha na kuratibu miradi na mipango ya maendeleo ya kijiji. Pia, watahiniwa 104,104 (7.71%) waliochagua kipotoshi B *Afisa maendeleo wa Kijiji*, hawakutambua kuwa afisa huyo anahamasisha, anaratibu na kusimamia maendeleo katika kijiji na watahiniwa 92,375 (6.84%) waliochagua kipotoshi D, *Jeshi la polisi* hawakuwa sahihi kwa mantiki kwamba licha ya jeshi la polisi kuwa ni chombo cha dola huwajibika kisheria na ulinzi wa raia na mali zao, haimaanishi kuwa jeshi hilo linaweza kulinda miundombinu yote katika kila kijiji nchi nzima. Hivyo, kila mwanajamii anao wajibu wa kulinda miundombinu iliyopo kwa ajili ya maendeleo ya jamii yake.


Mwisho, watahiniwa 41,818 (3.10%) waliochagua kipotoshi E, *Walimu na wazazi*, walishindwa kuelewa kuwa jukumu la kulinda miundo mbinu ya jamii katika kijiji sio tu la viongozi, walimu na wazazi peke yao bali ni la wanakijiji wote wakiwemo wafanyakazi wa umma, wazazi, viongozi, raia na vijana.

Swali la 17: Rasimali za taifa ni tunu zinazotakiwa kulindwa na kuhifadhiwa. Ni kundi lipi lina wajibu wa kulinda na kuhifadhi rasilimali za Taifa?

- A Maafisa wa polisi
- B Maafisa wa jeshi
- C Wananchi wote
- D Serikali ya kijiji
- E Viongozi wa serikali

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uelewa wa watahiniwa juu ya kubaini kundi lenye wajibu wa kulinda na kuhifadhi rasilimali za taifa. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 1,011,003 (74.85%) walijibu swalii hili kwa usahihi na watahiniwa 339,790 (25.15%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi C, *Wananchi wote* walielewa kuwa rasilimali za taifa ni vitu vilivyo katika mfumo wa fedha, vifaa au wafanyakazi ambavyo vipo

chini ya umiliki wa serikali au binafsi. Vitu hivyo hujumuisha ardhi, misitu, bahari, mito, ziwa, sehemu za kihistoria, milima, madini na wanyamapori. Rasilimali zote hizi ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa na vizazi vijavyo. Hivyo, ni jukumu la kila mwananchi kuzilinda na kuzihifadhi kwa njia mbalimbali ikiwamo kuepuka kuzihujumu, kutoa taarifa za watu wanaoziharibu kwenye mamlaka husika na kutunza mazingira. Chati Na. 17 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 17: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 17.


Kwa upande mwingine, watahiniwa 78, 292 (5.80%) waliochagua kipotoshi A, *Maafisa wa polisi*, watahiniwa 74.743 (5.53%) walichagua kipotoshi B, *Maafisa wa jeshi*, pia watahiniwa 60,187 (4.46%) walichagua kipotoshi D, *Serikali ya kijiji* na watahiniwa 114,176 (8.45%) walichagua kipotoshi E, *Viongozi wa serikali*. Makundi yote hayakujuua kuwa machaguo yote yanaundwa na watu ambao pia ni wananchi na wao kama raia wa nchi na wanalo jukumu la kulinda rasilimali bila kujali hadhi zao katika jamii ziwe za kiuchumi au kisiasa. Wakati huohuo, maafisa wa Polisi ni waajiriwa wa serikali ambao kazi yao ni kusimamia usalama wa raia na mali zao. Pia, Serikali ya kijiji ni mionganini mwa tawala katika serikali za mitaa ambao ni wa ngazi ya chini kabisa kimuundo ukitanguliwa na utawala wa kitongoji. Vilevile, Maafisa wa jeshi ni watu walioajiriwa katika Majeshi ya ulinzi na usalama. Aidha, viongozi wa serikali ni watu ambao hushikilia nyadhifa mbalimbali katika taasisi au

ofisi za umma ambao kimsingi wapo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi katika ngazi mbalimbali. Makundi haya yote yana wajibu wa kulinda na kuhifadhi rasilimali za taifa.

Swali la 18: Ni mbinu ipi utaitumia kuwafanya wanafunzi wenzako wajitolee kufanya kazi za shulen na nyumbani?

- A Kuwafundisha namna ya kufanya kazi
- B Kuwaadabisha ili wafanye kazi
- C Kuwahamasisha kufanya kazi
- D Kuwaonya ili wafanye kazi
- E Kuwaombea kwa Mungu

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uwezo wa mtahiniwa kutambua mbinu ambayo mwanafunzi anaweza kuitumia kuwafanya wenzake wajitolee kufanya kazi za shulen na nyumbani. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 777,357 (57.55%). walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 573,436 (42.45%) hawakujibu kwa usahihi. Jibu sahihi lilikuwa C, *Kuwahamasisha kufanya kazi*. Watahiniwa waliochagua jibu hili walitambua kwamba kuhamasisha watu ni kuwaandaa ili wawe tayari kushiriki katika kazi au tukio fulani kwa hiari yao chini ya usimamizi mdogo sana au pasipo kusimamiwa. Kwa mfano, shulen wanafunzi wanatakiwa kuhamasishwa ili wawe tayari kufanya kazi za shule bila ulazima wa kusimamiwa au kuwa na usimamizi mdogo. Hili linaweza kufanikiwa kwa kila mtu kujua madhumuni ya kufanya kazi fulani, kufanya kazi kama timu na kuwashirikisha katika uandaaji wa mikakati ya utekelezaji wa kazi husika. Yote haya yanafanywa ili kumjengea mtu tabia ya kujitolea kufanya kazi kwa hiari yake bila kulazimishwa. Chati Na. 18 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 18: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 18*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 352,513 (26.10%) walichagua kipotoshi A; *Kuwafundisha namna ya kufanya kazi*. Watahiniwa hao walitambua kuwa huo ni mchakato wa kumuwezesha mtu kufahamu njia na mbinu mbalimbali za kufanya kazi fulani kwa kutumia maarifa au ujuzi alionao. Hivyo, jibu hili halikuwa sahihi kwa sababu mtu anaweza kufundishwa namna ya kufanyakazi lakini bado akawa hana utayari wa kujitolea kufanya kazi hiyo. Kwa mfano shulenii wanafunzi hufundishwa namna ya kufanya kazi ndogondogo lakini bado baadhi yao hawana utayari wa kujitolea.

Pia, watahiniwa wengine 54,768 (4.05%) walichagua kipotoshi B, *Kuwaadabisha ili wafanye kazi*. Kuwaadabisha watu ni kitendo cha kuwalazimisha kuwa watiifu kwa kufuata taratibu zilizopo na kuwafanya kuwa na tabia njema. Hili pia halikuwa jibu sahihi kwa sababu mwanafunzi akiadabishwa humfanya afanye kazi sio tu kwa hiari yake bali kwa kuogopa asiadhibiwe. Vilevile, wapo watahiniwa 86,472 (6.40%) waliochagua kipotoshi D, *Kuwaonya ili wafanye kazi*. Watahiniwa hao hawakuwa sahihi kwani hawakujua kuwa kumuonya mtu ni kumjulisha, kumshauri au kumuashiria mtu kuhusu hatari, ubaya, madhara au jambo lolote baya ambalo linaweze kutokea wakati wowote kama tahadhari hazitazingatiwa. Kwa maneno


mengine, kuwaonya wanafunzi ili wafanye kazi ni kuwalazimisha kufanya kazi ili wasiadhibiwe. Hii inakatisha tama na utayari wa mwanafunzi kufanya kazi kwa hiari

Watahiniwa 66,749 (6.94%) walivutiwa na kipotoshi E, *Kuwaombea kwa Mungu*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa suala la kujitolea kufanya kazi sio suala la kiroho bali lina misingi yake katika familia, shule na jamii ambako mtoto hukulia na kujengeka katika misingi ya kupenda kazi mpaka anapokua.

Swali la 19: Mwongozo unaohusu mbinu za kupanga mipango ya maendeleo ya shule hutumiwa na nani?

- A Mwalimu mkuu
- B Mwalimu mkuu msaidizi
- C Uongozi wa shule
- D Serikali ya kijiji
- E Serikali ya kijiji

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii*. Watahiniwa walitakiwa kubaini mtu/kikundi chenye wajibu wa kutumia mwongozo wa mipango ya maendeleo ya shule katika ngazi ya shule ya msingi. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 499,171 (36.95%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 851,622 (63.05%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi D, *Kamati ya shule* walijua kuwa *Kamati ya shule* ina jukumu la kuandaa na kuidhinisha mipango ya maendeleo ya shule na mikakati ya utekelezaji wake. Vilevile, ina wajibu wa kuidhinisha na kusimamia matumizi bora ya fedha za maendeleo na uendeshaji wa shule. Aidha, kamati ya shule inawajibika kusimamia ujenzi na ukarabati wa madarasa, miundombinu na utunzaji wake, na miundombinu mingine. Chati Na. 19 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 19: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 19


Kwa upande mwingine, watahiniwa 547,508 (40.53%) waliochagua kipotoshi A, *Mwalimu mkuu*, hawakuwa sahihi kwa sababu mwalimu mkuu ni kiongozi na msimamizi wa shughuli zote za utawala katika shule. Pia, husimamia mtaala na tathmini ya maendeleo ya shule kitaaluma. Jukumu lingine ni kusimamia ustawi wa wanafunzi, nidhamu ya wafanyakazi na wanafunzi. Pia, watahiniwa 68,818 (5.09%) waliochagua kipotoshi B *Mwalimu mkuu msaidizi* hawakuwa na uelewa kuwa mwalimu mkuu msaidizi hupanga zamu za walimu, huwasimamia walimu wa taaluma, miradi, mazingira, uchumi na mipango, afya na nidhamu.

Aidha, watahiniwa 167, 483 (12.40%) waliochagua kipotoshi C, *Uongozi wa shule*. Hawakujua kwamba uongozi wa shule ni mfumo mzima wa utawala wa shule kuanzia Kamati ya shule, *Mwalimu mkuu*, walimu na viranja ambao kwa pamoja hushirikiana kuingoza shule kufikia malengo yake. Mwisho, watahiniwa 51,838 (3.84%) waliochagua kipotoshi E, *Serikali ya kijiji* hawakutambua kuwa kazi ya serikali ya kijiji ni kuhakikisha uwepo wa maendeleo kiuchumi na kijamii, ulinzi, amani, utulivu na utawala bora kijijini.

Swali la 20: Ni njia ipi **haiwezi** kuchochea maendeleo ya sekta mbalimbali?

- A Usimamizi wa biashara
- B Uchambuzi wa sera za uchumi
- C Usimamizi mzuri wa fedha
- D Uimarishwaji wa mazao ya chakula
- E Kuimarisha stadi za viwandani

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uelewa wa watahiniwa juu ya namna gani sekta mbalimbali zinaweza kuchochea maendeleo. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 336,425 (24.91%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 1,014,368 (75.09%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi D, *Uimarishwaji wa mazao ya chakula* walielewa kuwa mazao ya chakula ni kama nafaka (mahindi, mtama, mpunga) na mazao ya mizizi (muhogo, viazi) na mazao jamii ya kunde ambapo lengo mama ni kwa ajili ya matumizi ya kula, kwani huupa mwili nguvu, nishati na protini inayojenga mwili. Watahiniwa walielewa kuwa kuwepo kwa chakula pekee hakuwezi kuwa kichocheo cha maendeleo kwa sekta mbalimbali. Chati Na. 20 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Chati Na. 20: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 20*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 180,128 (13.33%) waliochagua kipotoshi A, *Usimamizi wa biashara* hawakujua

kwamba kuhusianisha shughuli mbalimbali za biashara na kuziratibu vizuri huwa ni kichocheo cha ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi. Hali kadhalika, watahiniwa 439,386 (32.53%) waliochagua kipotoshi B, *Uchambuzi wa sera za uchumi* hawakuwa sahihi kwa kuwa uchambuzi wa sera za uchumi huhusisha kufanya tathmini ya hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali katika kuendesha uchumi; kwa mfano sera ya fedha, sarafu, kodi, bajeti na utengenezaji wa ajira ambavyo kwa pamoja huchochea ukuaji wa uchumi katika sekta mbalimbali.


Aidha, watahiniwa 197,687 (14.63%) waliochagua kipotoshi C, *Usimamizi mzuri wa fedha* hawakuwa sahihi kwani usimamizi mzuri wa fedha huhusisha kukusanya, kupanga, kuratibu na kufuatilia matumizi sahihi ya fedha katika manunuzi na kutekeleza miradi ya maendeleo ni msingi wa ukuaji wa sekta yoyote. Bila usimamizi mzuri, fedha huweza kutumika vibaya na miradi ya maendeleo kutotekelzeza kama ilivyopangwa. Mwisho, watahiniwa 177,935 (13.17%) waliochagua kipotoshi E, *Kuimarisha stadi za viwandani* nao walikosea kwa sababu viwanda vyote, vikubwa na vidogo huhitaji wataalam katika uanzishwaji wake na hata uendeshaji wake. Kwa hiyo, ili kuwa na ufanisi katika uzalishaji wa bidhaa bora na utoaji wa huduma ni muhimu kuwa na wafanyakazi wenye ujuzi wa kutosha. Ujuzi wa viwanda ni pamoja na kufanya kazi kwa kushirikiana, utatuzi wa changamoto, kupanga na kuratibu, teknolojia na mawasiliano.

Swali la 21: Ni shughuli ipi ya binadamu huhifadhi rasilimali katika mazingira yetu?

- A Uoshaji wa madini kwa kutumia kemikali
- B Uchomaji wa misitu na nyasi
- C Kilimo cha mazao ya mzunguko
- D Kutumia baruti katika uvuvi
- E Kutupa takataka sehemu ya wazi

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uwezo wa watahiniwa kutambua shughuli ambayo huhifadhi

rasilimali katika mazingira yetu. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambao mionganii mwao watahiniwa 873,593 (64.67%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 477,200 (35.33%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi C, *Kilimo cha mazao ya mzunguko* walielewa kuwa kilimo cha mazao ya mzunguko ni mfumo wa kilimo ambao mkulima hulima mazao katika eneo kwa awamu kwa kila msimu na hii husababisha shamba/udongo kuhifadhi rutuba. Shughuli nyingine ambazo hulinda rasilimali katika mazingira yetu ni pamoja na kupanda miti, matumizi mapya ya taka, kilimo cha matuta na kilimo cha kontua. Chati Na. 21 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 21: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 21

Kwa upande mwingine, watahiniwa 183,182 (13.56%) waliochagua kipotoshi A, *Uoshaji wa madini kwa kutumia kemikali* hawakuwa sahihi kwani uoshaji wa madini kwa kutumia kemikali ni kitendo cha kusafisha madini yanayochimbwa ardhini kama vile dhahabu, almasi na kadhalika kwa kutumia dawa inayosababisha kitu kubadilika kikemikali. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa kemikali itumiwayo kuoshea madini huleta uhreibifu wa mazingira na ustawi wa viumbe anuwai. Watahiniwa 113,674 (8.42%) waliochagua kipotoshi B, *Uchomaji wa misitu na nyasi* hawakuwa sahihi kwa sababu uchomaji wa misitu na nyasi ni


kitendo cha kuunguza uoto wa asili. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa uchomaji wa misitu na nyasi huua viumbe hai vilivyomo kwenye ardhini, pia husababisha uchafuzi wa hewa na kuzalisha hewa ya ukaa ambayo athari yake ni kuchangia kuongezaka kwa joto ulimwenguni na hatimaye kuharibu rasilimali zinazotuzunguka.

Aidha, watahiniwa 61,447 (4.55%) waliochagua kipotoshi D, *Kutumia baruti katika uvuvi* hawakuwa sahihi kwa kutumia baruti katika uvuvi ni kitendo cha kutoa samaki baharini, ziwani au bwawani kwa kutumia milipuko au vilipuzi. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa matumizi ya baruti katika uvuvi ni hatari kwa mazingira kwani huharibu mazalia na kuua samaki na viumbe vingine ndani ya maji na kuchafua maji. Vilevile, watahiniwa 103,731 (7.68%) waliochagua kipotoshi E, *Kutupa takataka sehemu ya wazi* hawakuwa sahihi kwani kutupa takataka eneo la wazi ni kitendo cha kuacha uchafu katika eneo ambalo limetengwa kwa matumizi mengine kama vile michezo na maonesho mbalimbali. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kutupa takataka sehemu ya wazi hupelekea uchafuzi wa ardhi na hewa kwani baadhi ya takataka haziozi au kumeng'enyeka na pia baadhi yake kutoa harufu mbaya.

Swali la 22: Ofisa Mtendaji wa Kata ana majukumu yafuatayo **isipokuwa**

- A kusimamia shughuli zote za maendeleo katika kata.
- B kusimamia amani na usalama wa raia na mali.
- C kusimamia shughuli za uchaguzi katika eneo lake.
- D kuwa katibu wa vikao vyote katika eneo lake.
- E kuwawakilisha wananchi katika vikao vyatengenezwa.

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uelewa wa mtahiniwa kuhusu kazi za Ofisa Mtendaji wa Kata. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 274,398 (20.31%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 1,076,395 (79.69%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi E *kuwawakilisha wananchi katika vikao* vya serikali walibaini kwamba Ofisa Mtendaji wa Kata siyo mwakilishi wa wananchi bali ni mwajiriwa wa serikali kwa ajili ya kusimamia shughuli za maendeleo ya kata. Aidha, kazi ya uwakilishi wa wananchi hufanywa na Diwani wa Kata ambaye huchaguliwa na wananchi katika maeneo husika. Chati Na. 22 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Chati Na: 22: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 22


Hata hivyo, watahiniwa 143,531 (10.63%) walichagua kipotoshi A *kusimamia shughuli zote za maendeleo katika kata*. Watahiniwa wengine 500,684 (37.07%) walichagua kipotoshi B; *kusimamia amani na usalama wa raia na mali*. Vilevile, wapo watahiniwa wengine 194,330 (14.39%) waliochagua kipotoshi C, *kusimamia shughuli za uchaguzi katika eneo lake* na watahiniwa 219,097 (16.22%) walichagua kipotoshi D; *kuwa katibu wa vikao vyote katika eneo lake*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa Ofisa Mtendaji wa Kata huajiriwa na serikali na ni afisa anayehusika na usimamizi wa shughuli zote za serikali ikiwa ni pamoja na kusimamia watumishi wa umma kwa

niaba ya Mkurugenzi Mtendaji. Husimamia shughuli zote za uchaguzi na shughuli za maendeleo na hutunza kumbukumbu za vikao katika kata. Kwa hiyo hizo zote ni kazi za Ofisa Mtendaji Kata.

Swali la 23: Mwaisa hupenda kujifunza mambo yanayohusu mazingira. Mazingira yanaweza kutumikaje katika kujifunza?

- A Kujaribu nadharia B Kwa kudadisi
- C Kwa kuuliza maswali D Kwa kutumia maigizo
- E Kwa njia ya masimulizi

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* na lilimtaka mtahiniwa kutambua namna mazingira yanavyoweza kutumika katika mchakato wa kujifunza. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 404,664 (29.96%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 946,129 (70.04%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi B, *Kwa kudadisi* walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mazingira kuwa ni hali au mambo yanayokizunguka kiumbe katika sehemu au maisha yake. Aidha, mazingira yanaipa jamii vitu mbalimbali vinavyoweza kutumika katika mchakato wa kufundisha na kujifunza. Vitu hivyo vinaweza kuwa vya asili au vya kutengenezwa na binadamu. Mfano wa vitu hivyo ni ardhi, maji, hewa na vitu vyote vilivyomo. Vitu au zana hizo zinalenga kutumika kupata maarifa mbalimbali yaliyo na manufaa kwa binadamu. Vilevile watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa udadisi ni njia sahihi ya kujifunzia kutoka katika mazingira. Hii ni kwa sababu udadisi unahuishisha utafutaji wa jambo/taarifa kwa kuuliza, kwa kupeleleza, kuhoji, kutafiti, kupekua au kuchunguza kutoka katika mazingira. Chati Na. 23 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 23: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 23*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 346,821 (25.68%) waliochagua kipotoshi A, *Kujaribu nadharia* hawakuwa sahihi kwani kujaribu nadharia ni kupima mawazo/maelezo au muongozo uliopangwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa kujaribu nadharia haiwezi kutumika kama njia sahihi ya kuweza kujifunza kutoka katika mazingira kwani kitendo hiki hulenga kuthibitisha uhalisia wa nadharia. Kadhalika, watahiniwa 266,626 (19.74%) waliochagua kipotoshi C, *Kwa kuuliza maswali* hawakuwa sahihi kwa sababu kuuliza maswali kunaweza kusitoe matokeo yanayotarajiwa kama maswali hayo hayakutungwa kwa kuzingatia matakwa na lengo la kujifunza.


Vilevile, watahiniwa 165, 286 (12.24%) waliochagua kipotoshi D, *Kwa kutumia maigizo* hawakuwa sahihi kwani maigizo ni tungo za kisanaa ambazo huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo. Hata hivyo, maigizo yanaweza kuwa siyo njia yenye tija katika kujifunza, kwani hutoa nafasi kwa wahusika kuchunguza jambo kuondoa uhalisia, hivyo kupotosha ukweli. Pia, watahiniwa 149,203 (11.05%) waliochagua kipotoshi E, *Kwa njia ya masimulizi* hawakuwa sahihi kwa sababu masimulizi ni kutoa maelezo juu ya tukio fulani au kutoa habari/kusoma maandishi yanayo elezea tukio fulani kwa sauti. Watahiniwa hao hawakuelewa kwamba masimulizi hayawezi

kutoa taarifa zenyehu uhalisia kwani zinategemea mtazamo wa anayesimulia kuhusu jambo fulani.

Swali la 24: Kitendo cha kuhoji kila kitu katika mchakato wa ujifunza huitwaje?

- | | |
|------------|----------------|
| A Ubunifu | B Ustahimilivu |
| C Udadisi | D Uvumilivu |
| E Uadilifu | |

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* na lilipima maarifa ya watahiniwa kuhusu dhana ya kuchambua mambo kiyakinifu. Takwimu zinaonesha kuwa swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 943,686 (69.86%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 407,107(30.14%) hawakujibu kwa usahihi. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliochagua jibu sahihi C, *Udadisi* walielewa maana ya udadisi kuwa ni tabia ya kuchunguza kitu au jambo kwa kina au kutafuta ukweli kuhusu jambo fulani katika ujifunzaji. Chati Na. 24 unaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 24: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 24*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 144,251 (10.68%) waliochagua kipotoshi A, *Ubunifu* hawakuwa sahihi kwa sababu ubunifu ni kitendo cha kugundua au kutengeneza kitu kwa mara

ya kwanza. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa ubunifu sio njia ya kujifunza kwa kuhoji kila kitu. Vilevile, watahiniwa 90,130 (6.67%) waliochagua kipotoshi B, *Ustahimilivu* hawakuwa sahihi kwani ustahimilivu ni uwezo wa kuhimili mambo mazito bila ya kulalamika.


Aidha, watahiniwa 81,209 (6.01%) waliochagua kipotoshi D, *Uvumilivu* hawakuwa sahihi kwa kuwa uvumilivu ni hali/tendo la kuendelea na jambo licha ya kuwa na msukosuko na taabu; hii ni hali ya kuwa na subira. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa uvumilivu siyo njia ya kujifunza kwa kuhoji kila kitu. Pia, watahiniwa 78,230 (5.79%) waliochagua kipotoshi E, *Uadilifu* hawakuwa sahihi kwani uadilifu ni kuwa na tabia ya kutenda haki na kutokupendelea katika kufanya maamuzi yanayozingatia kanuni. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa uadilifu siyo njia ya kujifunza kwa kuhoji kila kitu. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, D na E, hawakuelewa dhana sahihi inayobeba tafsiri ya kitendo cha kuhoji kila kitu katika mchakato wa kujifunza.

Swali Ia 25: Ni kwanini inashauriwa kujenga hoja unapozungumzia jambo lolote?

- A Kuwaelekeza wengine kuhusu ujuzi wako.
- B Kuthibitisha uadilifu wako mbele ya watu.
- C Kuthibitisha usahihi wa majibu yako.
- D Kuthibitisha uwezo wako wa kuongea.
- E Kuthibitisha uelewa wako mbele ya watu

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuchambua mambo kiyakinifu. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 448,001 (33.17%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 902,792 (66.83%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi C; *Kuthibitisha*

usahihii wa majibu yako walielewa kwamba hoja ni maelezo yenye misingi na vigezo yanayotolewa kuthibitisha ukweli au uhalali wa jambo fulani. Hivyo, inaweza kuwa sababu au seti ya sababu ambayo kimsingi hulenga kuthibitisha kwa ushahidi wazo, kitendo au nadharia fulani kwa malengo ya kuwafanya watu wengine wakubali au wasikubali katika kitu/jambo linaloongelewa. Chati Na. 25 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Chati Na. 25: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 25


Hata hivyo, watahiniwa 338,975 (25.09%) waliochagua kipotoshi A, *Kuwaelekeza wengine kuhusu ujuzi wako na watahiniwa* 146,288 (10.83%) waliochagua kipotoshi B; *Kuthibitisha uadilifu wako mbele ya watu*. Machaguo haya hayakuwa majibu sahihi kwa sababu kipotoshi A, kilihusu kufundisha watu kuhusu umahiri wa mtu katika kufanya mambo fulani. Vilevile kipotoshi B, kilihusiana na kuwaonesha watu utiifu au usafi wa mtu kimaadili. Machaguo hayo hayakuwa na uhusiano wowote na uchambuzi wa mambo kiyakinifu. Vilevile, watahiniwa 83,596 (6.19%) waliochagua kipotoshi D; *Kuthibitisha uwezo wako wa kuongea na watahiniwa wengine* 314,212 (23.26%) na waliochagua kipotoshi E; *Kuthibitisha uelewa wako mbele ya watu*, hawakuwa sahihi kwa sababu kuthibitisha uwezo wa kuongea ni kitendo cha kuwaonesha watu ujuzi wa mtu kuwasiliana kwa mdomo kwa ufasaha. Pia, kuthibitisha uelewa wa mtu mbele ya watu humaanisha kitendo

cha kuwaonesha wengine kuwa unao ufahamu wa kina wa jambo fulani. Kwa muktadha huo, machaguo hayo hayakujikita katika kutoa vielelezo au sababu za kuthibitisha hoja na badala yake yanaashiria matendo ya kujiona na kujikweza ambayo hayajengi wala kudumisha tabia ya ustahimilivu katika jamii.

Swali la 26: Uvumilivu una faida gani katika maisha ya shule na nyumbani kwa mwanafunzi?

- A Kudumisha mitazamo ya mafanikio
- B Kumsaidia kujifunza mambo yaliyopita kiyakinifu
- C Kumsaidia kukubaliana na matarajio ya jamii
- D Kumsaidia kukubaliana na maamuzi ya walio wengi
- E Kujenga uhusiano mzuri na wenzake

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu*. Na mtahiniwa alitakiwa kubainisha faida anayopata kwa kuwa mvumilivu katika maisha ya shulenii na nyumbani. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 521,873 (38.63%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 828,920 (61.37%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi E, *Kujenga uhusiano mzuri na wenzake*, walifahamu kwamba mvumilivu ni mtu mwenye uwezo wa kustahimili changamoto za maisha bila kukata tamaa. Pia wanafunzi hawa walifahamu kuwa uvumilivu una faida mbalimbali katika maisha kama vile kusaidia kufikia malengo mtu aliyojiwekea, kujenga utayari wa mtu kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa kutumia njia sahihi, kujenga afya ya akili, kujifunza mambo mapya, kufanya maamuzi sahihi na kujenga mahusiano mazuri na wengine. Chati Na. 26 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Chati Na. 26: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 26


Kwa upande mwingine, watahiniwa 395,378 (29.27%) walichagua kipotoshi A; *Kudumisha mitazamo ya mafanikio*. hawakutambua kuwa kudumisha mitazamo ya mafanikio hujumuisha kujitolea kwa nguvu na moyo wote ili kufanikisha jambo fulani licha ya vikwazo au changamoto anazokutana nazo mtu. Mwelekeo wa mafaniko unaweza kupatikana kwa kuzingatia misingi na mambo mbalimbali kama vile: kuwa na imani kuhusu uwezekano wa kufanikiwa, kujitolea, kujitegemea, uthubutu wa kuanza kufanya kazi na kukua au mjongeo. Chaguo hili halikuwa jibu sahihi kwa sababu kuwa na mitazamo ya mafanikio siyo lazima iambatane na uvumilivu mara zote na wakati mwingine kiu ya mafanikio huondoa uvumilivu na kupelekea watu kutumia njia zisizo halali kuhakikisha wanafanikiwa katika jambo fulani. Vilevile, watahiniwa 184,737 (13.68%) walichagua kipotoshi B; *Kumsaidia kujifunza mambo yaliyopita kiyakinifu*. Chaguo hili pia halikuwa sahihi kwa sababu halikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na faida za uvumilivu. Kwa mfano, mwanafunzi hahitaji kuwa mvumilivu ili aweze kujifunza mambo yaliyopita kiyakinifu bali anahitaji zaidi maarifa ya uyakinifu ili aweze kudadavua taarifa na matukio mbalimbali ya kihistoria. Vilevile, watahiniwa 122,946 (9.10%) walichagua C; *Kumsaidia kukubaliana na matarajio ya jamii*, na watahaniwa 106,475 (7.88%) waliochagua kipotoshi D; *Kumsaidia kukubaliana na*

maamuzi ya walio wengi. Machaguo haya hayakuhusiana na faida za uvumilivu kwa mwanafunzi bali yalihu kukubaliana na matokeo na kupenda kuithamini jamii, hivyo hayakuwa majibu sahihi.

Swali la 27: Ni kwa namna gani tabia ya utoro kwa wanafunzi inaweza kukomeshwa shulen?

- A Kukubali makosa na kuomba msamaha
- B Kujifunza kutokana na makosa na kujirekebisha
- C Kuwakimbia walimu na kujificha
- D Viongozi wa serikali kuingilia katika
- E Kukubali makosa ili kujenga uaminifu

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu*. Katika swalii hili, watahiniwa walitakiwa kubaini njia bora inayoweza kutumika kuzuia utoro wa wanafunzi shulen. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 607,209 (44.95%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 743,584 (55.05%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi B, *Kujifunza kutokana na makosa na kujirekebisha* walielewa kuwa kujifunza kutokana na makosa na kujirekebisha hufanya mwanafunzi kuelewa kosa alilotenda na kujirekebisha ili asirudie tena. Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kwa walimu kuwashauri wanafunzi kuhusu madhara ya utoro na kuwaonya dhidi ya tabia zisizokubalika. Chati Na. 27 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.



Chati Na. 27: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 27

Kwa upande mwingine, watahiniwa 266,699 (19.74%) waliochagua kipotoshi A, *Kukubali makosa na kuomba msamaha* na watahiniwa 176,401 (13.06%) waliochagua E, *Kukubali makosa ili kujenga uaminifu* hawakuwa sahihi kwa sababu kukubali tu makosa siyo suluhisho la mwanafunzi kukoma tabia fulani. Pia, kuomba msamaha na kujenga uaminifu baada ya kuonesha tabia isiyofaa siyo uthibitisho kwamba mwanafunzi ataacha vitendo hivyo kwani anaweza kukubali makosa na kujenga uaminifu ili asitiliwe mashaka na kufuatiliwa. Kwa hiyo, chaguzi zote mbili hazikuwa njia sahihi za kuondoa vitendo visisvyokubalika kama utoro shulenii.


Aidha, watahiniwa 96,003 (7.11%) waliochagua kipotoshi C, *Kuwakimbia walimu na kujificha* hawakuwa sahihi kwani hii ni namna nyingine ya utovu wa nidhamu. Katika hali ya kawaida, wanafunzi wanatakiwa kuheshimu, kuthamini na kuwatii walimu maana ni sehemu ya walezi wao. Uhustiano mzuri kati ya mwalimu na mwanafunzi huchochea upendo na hali ya kukubalika baina yao. Mahusiano hayo yanaweza kufanya mwanafunzi kuacha tabia mbaya kama vile utoro na kuimarisha ubora wa kitaaluma. Mwisho, watahiniwa 188,238 (13.94%) waliochagua kipotoshi D, *Viongozi wa serikali kuingilia* kati hawakuwa sahihi kwa sababu utoro pamoja na tabia nyingine zisizokubalika zinahitaji dhamiri na moyo wa mwanafunzi

mwenyewe kuacha huku wakisimamiwa na kuongozwa na walimu wao kwani wana ujuzi wa malezi na makuzi. Zoezi hili huwa na matokeo chanya walimu wakishirikiana na wazazi wa wanafunzi husika. Kazi ya viongozi wa serikali ni kutengeneza mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuleta fedha za kuendesha shule, kutengeneza miundombinu ya shule na kuajiri wafanyakazi.

Swali la 28: Ni kwa nini ni muhimu kwa wanafunzi kuuliza maswali wakati wa vipindi darasani?

- A Kuweza B Kuweza kujulikana
 kufundishana
- C Kuweza kupata D Kudumisha
 ufanuzi nidhamu ya darasa
- E Kuwafurahisha
 walimu

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu*. Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kubaini umuhimu wa wanafunzi kuuliza maswali wakati wa vipindi darasani. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 1,014,511 (75.10%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 336,282 (24.90%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi C, *Kuweza kupata ufanuzi* walielewa kwamba mawasiliano bayana kati ya mwalimu na mwanafunzi huchochaea mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwanafunzi akiuliza swali wakati wa kipindi humfanya mwalimu kupata mrejesho kuhusu ufanisi wa mchakato wa ujifunzaji. Hivyo kuwa katika nafasi nzuri ya kuongeza maelezo ya ziada na kutoa mifano zaidi ili somo lieleweke. Kwa ujumla, kuuliza maswali ni chachu ya wanafunzi kufikiri, kujenga hoja na kuchanganua mambo kiyakinifu, ili kupata ujuzi na kuondoa utata kwa maeneo ambayo hayakueleweka hasa pale swali linapojibiwa. Chati Na. 28 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.



Chati Na: 28: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 28

Kwa upande mwingine, watahiniwa 143,242 (10.60%) waliochagua kipotoshi A, *Kuweza kufundishana*, hawakuwa sahihi kwa sababu kufundishana ni sehemu ya mchakato wa ujifunzaji na kunaweza kufanyika kwa njia mbalimbali kama vile majadiliano katika makundi, midahalo, kufanya kazi mradi za kitaaluma pamoja na kufanya mazoezi ya kitaaluma na marafiki. Hivyo chaguo hili halina uzito wa kutosha kustahili kuwa jibu sahihi. Watahiniwa 56,441 (4.18%) waliochagua kipotoshi B, *Kuweza kujulikana*, hawakuwa sahihi kwasababu wanafunzi huwa hawaulizi maswali ili wajitambulisse au wapate umaarufu. Walimu makini hutakiwa kuwafahamu wanafunzi wao kwa majina, tabia na uwezo. Mwanafunzi akiuliza swali kwa lengo la kujipatia umaarufu anakuwa anaonesha tabia isiyofaa katika jamii.


Vilevile, watahiniwa 72,866 (5.39%) waliochagua kipotoshi D, *Kudumisha nidhamu ya darasa*, hawakuwa sahihi kwa sababu ni jukumu la walimu kulinda nidhamu ya wanafunzi ndani na nje ya madarasa. Hivyo, kipindi cha maswali na majibu hakina lengo la kudumisha heshima ya darasa bali kuboresha ujifunzaji unaomlenga mwanafunzi. Mwisho, watahiniwa 53,107 (3.93%) waliochagua E, *Kuwafurahisha walimu* nao walikosea kwa sababu kuuliza swali ni hatua muhimu katika ufundishaji wa somo kwa kuwa ni mbinu inayomlenga mwanafunzi na kupata

ushiriki wa wanafunzi wakati wa kufundisha. Walimu hufurahishwa na tabia nzuri zinazooneshwa na wanafunzi pamoja na moyo wa kujituma kujifunza.

Swali la 29: Vyando gani vyaa taarifa vinaweza kumsaidia mwanafunzi kufanya vizuri katika mitihani yake?

- A Kusikiliza redio na kujisomea vitabu
- B Kuangalia runinga na sinema
- C Kusikiliza hadithi na kujisomea
- D Kucheza michezo na kusoma magazeti
- E Kusoma magazeti na kuimba nyimbo

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu*. Swali lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu vyando sahihi vyaa taarifa vinavyoweza kumsaidia mwanafunzi kufanya vizuri katika mitihani. Swali lilijibwa na watahiniwa 1,350,793 na uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 694,056 (51.38%) walijibu kwa usahihi. Jibu sahihi lilikuwa A, *Kusikiliza redio na kujisomea vitabu*. Watahiniwa walijua kuwa redio huwa na vipindi mbalimbali vyenye makala za kitaaluma na taarifa nyingine ambazo ni muhimu kwa mwanafunzi. Aidha, kusoma vitabu ni njia ya uhakika zaidi ya kupata taarifa na maarifa kwani kila somo huwa na vitabu vyaa ziada na kiada ambavyo vinaweza kutumika na wanafunzi kujisomea wakati wa maandalizi ya mitihani. Chati Na. 29 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.



Chati Na. 29: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 29

Kwa upande mwingine, watahiniwa 72,983 (5.40%) waliochagua kipotoshi B, *Kuangalia runinga na sinema* hawakuwa sahihi ingawa chaguo hili lilikuwa na runinga ambayo ni msaada kwa mwanafunzi kupata taarifa kwani huwa na vipindi vyenye kuelimisha kama vile habari na makala mbalimbali. Kuwepo kwa sinema kulifanya chaguo hili lisiwe jibu sahihi kwa sababu sinema huhusisha filamu ambazo huoneshwa katika kumbi maalumu kwa minajili ya watu kuburudika. Hivyo haifai kuwa chanzo cha taarifa kwa wanafunzi wanaojiandaa na mitihani. Pia maudhui mengine yanayooneshwa kwenye sinema hayafai kwa wenye umri mdogo. Hali kadharika, watahiniwa 488,130 (36.14%) waliochagua kipotoshi C, *Kusikiliza hadithi na kujisomea* hawakuwa sahihi ingawa chaguo lilikuwa na kujisomea ambayo ni moja ya njia kuu za kujandaa kwa ajili ya mitihani. Kujisomea humfanya mwanafunzi kupitia mihtasari, nukuu na rejea mbalimbali ili kupata habari na kukazia maarifa kwa ajili ya mitihani. Aidha, kusikiliza hadithi kulilifanya chaguo hili lisiwe jibu sahihi kwani siyo kila hadithi ni ya kitaaluma. Pia, hadithi haiwezi kuwa chanzo cha taarifa cha kutegemewa na wanafunzi kwa sababu mara nyingine huwa ni za kubuni, na hupoteza ukweli pale anayesimulia anaposahau baadhi ya mambo au kuongeza chumvi.


Vilevile, watahiniwa 44,822 (3.32%) waliochagua kipotoshi D, *Kucheza michezo na kusoma magazeti* na watahiiwa 38,966 (2.88%) waliochagua E, *Kusoma magazeti na kuimba nyimbo* pia hawakuwa sahihi ingawa zilihusisha kusoma magazeti. Magazeti hasa yale yanayoandika habari zenye kuelimisha na makala mbalimbali yanaweza kuwa msaada kwa wanafunzi kupata habari na kuongeza maarifa. Hata hivyo, machaguo yote mawili hayakuwa sahihi kwa kuwa yalihusisha kucheza michezo, ambayo huwa ni kwa ajili ya kujenga utimamu wa mwili na akili na hivyo siyo chanzo cha taarifa. Pia, kuimba nyimbo ni njia mojawapo inayoweza kutumika katika ufundishaji

lakini sio chanzo cha taarifa kinachoweza kumsaidia mwanafunzi katika mitihani hasa anapotaka kujikumbusha aliyojifunza siku za nyuma. Inawezekana mwanafunzi kupata ujumbe fulani kuititia kusikiliza nyimbo. Hata hivyo, siyo kila wimbo una mafunzo ndani yake kwani nyingine hulenga kuburudisha tu. Kiuhalisia baadhi ya nyimbo zina ujumbe ambaao siyo sahihi kwa vijana.

Swali la 30: Kauli ipi kati ya zifuatazo inaeleza hali ya uadilifu?

- A Kutokekua maadili katika jamii
- B Kuishi kwa kufuata mawazo binafsi
- C Kuishi kwa kufuata miongozo ya viongozi
- D Kuishi kwa kufuata maadili ya jamii
- E Kuishi kwa kufuata makundi rika

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa mwadilifu* na lilipima maarifa ya watahiniwa kuhusu mazingira mbalimbali yanayoashiria hali ya uadilifu. Swali lilijibwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 746,437 (55.26%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 233,670 (17.3%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliobaini jibu sahihi D, *Kuishi kwa kufuata maadili ya jamii* walielewa kuwa uadilifu ni hali ya kuishi kwa kufuata maadili ya jamii kama vile uwajibikaji, uwazi, uaminifu na utii. Matendo yote haya ni misingi ya kijamii ambayo inaweza kuwa mizuri au mibaya. Vilevile, watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa maadili ya jamii ni vigezo vya tabia njema katika jamii kama vile mwenendo mwema, uaminifu na usawa. Uadilifu chimbuko lake ni katika jamii na siyo marafiki tu, mtu binafsi au viongozi. Chati Na. 30 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 30: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 30

Kwa upande mwingine, watahiniwa 140,257 (10.38%) waliochagua kipotoshi A, *Kutokufuata maadili katika jamii* hawakuwa sahihi kwani ni kitendo cha kutokuzingatia vigezo vya tabia njema katika jamii. Watahiniwa hao hawakuelewewa kuwa, maadili yaliyowekwa katika jamii huhusisha pia uaminifu na vigezo vya tabia njema ikiwa ni pamoja na uadilifu. Pia, watahiniwa 131,230 (9.72%) waliochagua kipotoshi B, *Kuishi kwa kufuata mawazo binafsi* hawakuwa sahihi kwa sababu mawazo binafsi ni maarifa na ujuzi alionao mtu kutokana na juhudhi binafsi na siyo kwa kuelekezwa. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kuishi kwa kufuata mawazo binafsi hakuakisi mara zote uadilifu kwani mawazo ya mtu binafsi wakati mwingine huambatana na ubinafsi kwa kuzingatia sababu alizonazo. Hivyo uadilifu unawezekana iwapo misingi iliyowekwa na jamii inafuatwa.


Aidha, watahiniwa 242,925 (17.98%) waliochagua kipotoshi C, *Kuishi kwa kufuata miongozo ya viongozi* hawakuwa sahihi kwani miongozo ya viongozi ni maelekezo ya wafanya maamuzi au wasimamizi wa kundi. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa viongozi si mara zote wanatoa miongozo au maelekezo yanayozingatia uadilifu kwani wanaweza kupendelea au kutoa maelekezo yenye uadilifu wa kutiliwa mashaka. Katika hili, viongozi pia kama sehemu ya jamii hupaswa kuishi kwa kufuata

maadili yaliyopo katika jamii. Vilevile, watahiniwa 72,835 (5.39%) waliochagua kipotoshi E, *Kuishi kwa kufuata makundi rika* hawakuwa sahihi kwa kuwa makundi rika ni mkusanyiko wa watu wenye takribani umri mmoja au nafasi sawa katika jamii au uwezo sawa. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa makundi rika huwa na mitazamo na maslahi yanayofanana tofauti na makundi mengine katika jamii. Hivyo kusababisha mtu kupoteza mwelekeo kwa kufuata tabia na mwenendo usiofaa kwa jamii kwa ujumla. Ukweli ni kwamba baadhi ya makundi rika yana ushawishi potofu kwa washirika wa kundi rika.

Swali Ia 31: Matata ni mwizi lakini hujifanya ni mzuri anapokutana na rafiki yake Kamote na hulaani wenye tabia hiyo. Je ni neno lipi linalezea tabia anayoionesha Matata kwa rafiki yake ?

- | | |
|----------------|--------------------|
| A Unafiki | B Usaliti |
| C Ujasiri | D Uwajibikaji |
| E Uwazi | |

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa mwadilifu* na lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu dhana ya kuaminika katika jamii. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 896,210 (66.35%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 454,583 (33.65%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliobaini jibu sahihi A, *Unafiki* walikuwa na uelewa kuwa unafiki ni tabia isiyoafikiana na kitu au jambo analoliamini. Unafiki hujidhirisha pale mtu anaye ongea uongo au jambo lisilo na uhalisia anapotoa ahadi ambayo hawezi kutimiza, ila wakati wote anapoaminiwa huthibitisha kuwa ni mkweli. Chati Na. 31 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 31: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 31


Kwa upande mwingine, watahiniwa 221,153 (16.37%) waliochagua kipotoshi B, *Usaliti* hawakuwa sahihi kwani usaliti ni kitendo cha kukosa utii au uaminifu kwa nchi/mtu aghalabu kwa kufanya jambo la kudhuru kwa kuwasaidia maadui. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa usaliti hauhusiani na tukio la tabia ya Matata ya unafiki na siyo usaliti. Pia, watahiniwa 93,969 (6.96%) waliochagua kipotoshi C, *Ujasiri* hawakuwa sahihi kwa sababu ujasiri ni hali ya kukabili jambo bila ya hofu; ni hali ya uhodari au ushujaa. Watahiniwa hao walikosa maarifa juu ya tendo la ujasiri kwani tukio la Matata halihusiani na tendo la ujasiri.

Vilevile, watahiniwa 63,112 (4.67%) waliochagua kipotoshi D, *Uwajibikaji* na watahiniwa 63,581 (4.71%) waliochagua kipotoshi E, *Uwazi* wote hawakuwa sahihi kwa kuva vipotoshi hivi viwili vyote ni misingi ya demokrasia na utawala bora. Kwa upande wa uwajibikaji ni hali ya kukosa hiari katika kufanya jambo. Katika dhana ya demokrasia uwazi ni hali ambayo raia wanapata taarifa mbalimbali juu ya serikali yao na hivyo kuweza kufanya maamuzi ya kisiasa. Watahiniwa hao walikosa uelewa wa maana ya maneno uwajibikaji na uwazi na hivyo kushindwa kuhusianisha tukio lililodhahirisha tabia ya Matata na jibu sahihi.

Swali la 32: Mitandao ya kijamii ni nyenzo ambayo kama haitatumika vizuri inaweza kuharibu jamii. Ipi ni njia sahihi ya kuzuia athari za mitandao kwa jamii?

- A Kufuata misingi ya maadili
- B Kuzima mawasiliano
- C Kutumia kwa nyakati chache
- D Kutumia taarifa kama zinavyotolewa
- E Kutumia faraghani

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa mwadilifu* na lilitaka mtahiniwa abainishe njia sahihi ya kuzuia athari za mitandao ya kijamii katika jamii. Swali lilijibwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 758,216 (56.13%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 592,577(43.87%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliobaini jibu sahihi A, *Kufuata misingi ya maadili* walifahamu kuwa mitandao ya kijamii ni tovuti au mfumo wa mawasiliano ya kiteknolojia unaotumiwa na watu kutafuta na kupeana taarifa kuitia vifaa mbalimbali kama vile simu na kompyuta. Taarifa hizo zinaweza kuwa ujumbe mfupi wa maneno, picha na video. Pia, watahiniwa hao walikuwa na maarifa kuwa baadhi ya taarifa zipatikanazo mitandaoni huweza kuathiri mitazamo ya kimaadili ya mtu au watu wa jamii husika kwa kuwaimarisha au kuwabomoa kijamii, kisiasa, kiuchumi au kitamaduni. Vilevile, watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa kufuata misingi ya maadili ambayo hushabihi tabia njema/inayokubalika itawawezesha wanajamii kupinga/kukataa maovu na kukumbatia mambo mema kutoka mitandaoni. Chati Na. 32 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 32: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 32*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 133,960 (9.92%) waliochagua kipotoshi B, *Kuzima mawasiliano* hawakuwa sahihi kwani kuzima mawasiliano ni kitendo cha kutoruhusu teknolojia ya mawasiliano kutumika kutoa na/au kupokea taarifa, mawazo, mitazamo na hisia. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa pamoja na matokeo hasi ya mitandao ya kijamii, mitandao ya kijamii ina matokeo chanya ambayo hunufaisha jamii kisiasa, kuchumi, kiutamaduni na kijamii. Pia, watahiniwa 97,173 (7.19%) waliochagua kipotoshi C, *Kutumia kwa nyakati chache* hawakuwa sahihi kwa sababu kutumia mitandao ya kijamii kwa nyakati chache kutakuwa ni kikwazo kwa wale wote wenye nia ya kupata taarifa za kuelimisha na taarifa nyingine muhimu kama za kibiashara na kifedha. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa maudhui yasiyofaa hutumwa mitandaoni muda wote.


Aidha, watahiniwa 270,239 (20.01%) waliochagua kipotoshi D, *Kutumia taarifa kama zinavyotolewa* hawakuwa sahihi kwa kuwa kutumia taarifa kama zinavyotolewa kunaweza kuharibu maadili ya jamii kwani baadhi ya taarifa kutoka mitandao ya kijamii haziendani na maadili ya jamii husika. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa matumizi ya mitandao hupelekeea muingiliano wa tamaduni na taarifa zinazorushwa mitandaoni; zinaweza kufaa au zisifae kulingana na maadili ya jamii husika.

Kadhalika, watahiniwa 75,459 (5.59%) waliochagua kipotoshi E, *Kutumia faraghani* hawakuwa sahihi kwa sababu kutumia mitandao ya kijamii faraghani ni matumizi ya mitandao mtu akiwa peke yake au sirini. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa taarifa au mambo yasiyofaa kutoka mitandaoni yanaweza kumuathiri mtumiaji hata kama atatumia kwa siri. Hivyo, matumizi ya mitandao ya kijamii iwe yanatumika na umma au kwa siri lazima yachunguzwe kwa umakini ili kuiepusha jamii na taarifa zisizofaa.

Swali la 33: Kila binadamu anayo haki ya kumiliki Mali. Haki hii inapatikana katika kundi gani la haki za binadamu?

- | | |
|-------------------------|-----------------------|
| A Kiuchumi na kijamii | B Kisiasa na kiuchumi |
| C Kijamii na kiraia | D Kiraia na kisiasa |
| E Kiutamaduni na kiraia | |

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa Mwadilifu* na liliwataka watahiniwa kubaini kundi ambalo haki ya kumiliki mali inapatikana. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 622,724 (46.10%) walijibu swal hili kwa usahihi na watahiniwa 728,069 (53.90%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi A, *Kiuchumi na kijamii* walikuwa na uelewa kwamba haki ya kiuchumi inajenga mazingira muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi kwa kila mtu. Haki ya kiuchumi inahusisha haki nyingine kama vile, haki ya kufanya kazi, haki ya ujira na haki ya kuijunga na vyama vya wafanyakazi. Vilevile, haki ya kijamii ni haki ambayo inatoa mazingira yanayowawezesha watu kuishi maisha mazuri. Haki hizo ni kama vile kuwa na afya, malazi, chakula na haki ya elimu. Kwa hiyo, haki ya kiuchumi na kijamii huwapa watu uhakika wa kumiliki mali zinazoshikika na zisizoshikika. Chati Na. 33 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.



Chati Na. 33: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 33


Kwa upande mwingine, watahiniwa 331,460 (24.54%) waliochagua kipotoshi B, *Kisiasa na kiuchumi*, hawakuwa sahihi kwani kipotoshi hiki kilihusisha haki za kisiasa. Watahiniwa hawa hawakuelewa kwamba haki za kisiasa ni haki zinazolinda uhuru wa kujieleza, uhuru wa kukutana na watu na uhuru wa kugombea na kupiga au kupigiwa kura katika chaguzi huru na za haki.

Vilevile, watahiniwa 181,884 (13.46%) waliochagua kipotoshi C, *Kijamii na kiraia*, watahiniwa 91,697 (6.79%) waliochagua D, *Kiraia na kisiasa* na watahiniwa 108,481 (8.03%) waliochagua E, *Kiutamaduni na kiraia* wote hawakuwa sahihi kwani vipotoshi hivyo vilihusisha haki za kiraia. Watahiniwa hawa hawakujua kwamba haki za kiraia zinahusu hasa haki ya kuishi, kuwa na uhuru binafsi, haki ya faragha, haki ya kulindwa dhidi ya mateso na manyanyaso, haki ya kutembea na kusafiri, haki ya uhuru wa mawazo, haki ya imani na haki ya kuabudu katika dini. Vilevile, haki za kiutamaduni zilizokuwa katika kipotoshi E, *Kiutamaduni na kiraia* ambacho hakikuwa sahihi kwani haki za kiutamaduni hazihusiani na kumiliki mali ikilinganishwa na haki za kiuchumi. Haki za kiutamaduni huhusisha hasa haki ya kushiriki katika mambo ya kiutamaduni katika jamii na haki ya kuwa na hisa zinazotokana na ubunifu wa kisayansi, fasihi au uzalishaji wa sanaa yoyote.

Swali la 34: Kwa namna gani balozi anaweza kudumisha uhusiano mzuri kati ya Tanzania na nchi anayoiwakilisha?

- A Kuwa na ustahimilivu
- B Kutoa fursa za biashara
- C Kuwa na dhamira thabiti
- D Kutoa fursa za masomo
- E Kutoa misaada ya kifedha

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kudumisha Amani* na liliwapima watahiniwa kuhusu ufahamu wa uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine. Swali lilijibwa na watahiniwa 1,350,793. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 302, 211 (22.37%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 1,048,582 (77.63%) hawakujibu kwa usahihi. Waliochagua jibu sahihi C; *Kuwa na dhamira thabiti* walifahamu kuwa dhamira thabiti ni hali ya kujitoa kwa moyo na nguvu zote katika kutekeleza au kutimiza jambo au kazi fulani. Balozi ana wajibu wa kutekeleza mapatano kati ya nchi mbili katika mahusiano ya kidiplomasia kwa uwazi na kufanya shughuli zote kwa ufasaha na kwa kuwajibika. Majukumu hayo ni pamoja na kukuza maslahi ya kiuchumi ya Tanzania kwa njia mbalimbali kama vile biashara na utalii. Pia, kudumisha uhusiano wa kijamii na kiutamaduni kati ya Tanzania na nchi zingine, kuimarisha mahusiano na ushirikiano wa mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyopo Tanzania na nchi wenyeji na kuimarisha uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine katika nyanja nyingine kama vile elimu na teknolojia. Chati Na. 34 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




Chati Na. 34: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 34

Hata hivyo, watahiniwa 410,802 (30.41%) walichagua kipotoshi A; *Kuwa na ustahimili vu*. Mstahimillivu ni mtu mwenye uwezo wa kuvumilia, kuhimili na kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazomkabili. Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na uelewa juu ya mambo ya msingi yanayojenga mahusiano mazuri baina ya Tanzania na nchi nyingine. Pia, watahiniwa wengine 346,170 (25.63%) walichagua B; *Kutoa fursa za biashara*, watahiniwa 139,437 (10.32%) walichagua D; *Kutoa fursa za masomo* na watahiniwa 134,069 (9.93%) walichagua kipotoshi E; *Kutoa misaada ya kifedha*. Machaguo haya hayakuwa majibu sahihi kwa sababu ufanisi wake hutegemea dhamira thabiti ya balozi husika. Aidha, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa waliochagua majibu yasiyo sahihi hawakufahamu njia mbalimbali zinazotumiwa na balozi kudumisha uhusiano mzuri wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi zingine. Baadhi ya njia hizo ni: kufanya majadiliano ya mara kwa mara hasa panapotokea kutoelewana katika baadhi ya mambo, kuwa na dhamira thabiti ya kutekeleza mambo ambayo nchi mbili zanazohusiana kibalozi zimekubaliana na kudumisha uaminifu ili kuweza kujenga hali ya kuaminiana wakati wa kupanga, kujadili na kutekeleza mambo mbalimbali. Na mwisho kutumia diplomasia katika kutatua migogoro na kudumisha mawasiliano kwa viongozi wa nchi mbili kutembeleana na kubadilishana uzoefu.

Swali la 35: Kwanini watu waadilifu hupendwa na kuaminiwa katika jamii?

- A Hujijali na kuwa nadhifu
- B Wana maadili mema na hujali wengine
- C Huonesha utiifu na uvumilivu
- D Wanaonesha furaha na ustahimilivu
- E Wana maadili na ukarimu kwa wazee

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kuwa mwadilifuu* na lilipima uelewa wa watahiniwa wa kubaini sifa za watu waadilifu ambazo zinawafanya wapendwe na kuaminiwa katika jamii. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 na uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 872, 470 (64.59%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 478,323 (35.41%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa walioweza kubaini jibu sahihi B, *Wana maadili mema na hujali wengine* walielewa kuwa uadilifu ni hali ya kutenda haki bila kupendelea upande wowote. Pia, walielewa kuwa mtu mwenye uadilifu huishi kulingana na maadili ya jamii husika na huwa ni mtu wa kujali wengine. Chati Na. 35 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 35: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 35

Kwa upande mwingine, watahiniwa 90,638 (6.71%) waliochagua kipotoshi A, *Hujijali na kuwa nadhifu* hawakuwa sahihi kwa sababu kujiali na kuwa nadhifu ni matendo ambayo

yanamlenga mtu binafsi yeye mwenyewe na siyo uhusiano wake na wanajamii wengine. Kujijali ni kuchukua hatua za kujihifadhi na kudumisha ustawi wako na furaha yako binafsi. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa uadilifu ni zaidi ya mambo ya mtu binafsi.


Vilevile, watahiniwa 238,489 (17.51%) waliochagua kipotoshi C, *Huonesha utiifu na uvumilivu*; watahiniwa 68,301 (5.06%) waliochagua kipotoshi D, *Wanaonesha furaha na ustahimilivu na* watahiniwa 69,606.(5.15%) waliochagua kipotoshi E, *Wana maadili na ukarimu kwa wazee* hawakuwa sahihi kwa sababu vipotoshi hivi vyote huonesha baadhi ya vipengele vya sifa za maadili mema katika jamii. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu uadilifu ambao unahusisha maadili mema na yanayokubalika katika jamii sambamba na kuwajali wengine. Na hii husababisha watu waadilifu kupendwa na kuaminiwa.

Swali la 36: Mojawapo ya changamoto katika Umoja wa Afrika ni migogoro isiyoisha. Ni njia ipi inaweza kutumika katika kutatua migogoro hiyo?

- A Kuwa na jeshi moja
- B Kuondoa umaskini na utu
- C Kupambana na rushwa na uzalendo
- D Kuanzisha balozi katika nchi husika
- E Kuheshimu haki za binadamu

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kudumisha Amani* na lilimtaka mtahiniwa kubaini njia inayoweza kutumika kutatua migogoro katika Bara la Afrika. Swali lilijibwa na watahiniwa 1,350,793 na uchambuzi unaonesha kuwa kati ya hao, watahiniwa 621,866 (46.04%) walijibu swalii hili kwa usahihi na watahiniwa 728,927 (53.96%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa walioweza kubaini jibu sahihi E, *Kuheshimu haki za binadamu* walikuwa na uelewa juu ya dhana ya migogoro kuwa ni hali ya kutoafikiana katika mitazamo/misimamo au kanuni baina ya pande mbili. Aidha, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa dhana ya utatuzi wa migogoro kuwa ni mchakato

unaotumika kurejesha amani na utulivu baina ya pande mbili zinazotofautiana. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa juu ya uwepo wa migogoro Barani Afrika katika nchi kama Jamhuri ya Kideokrasia ya Kongo, Somalia na Sudani ya Kusini. Vilevile, watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa ukiukwaji wa haki za kisasa, kuchumi na kijamii huchochea migogoro Barani Afrika, hivyo ulinzi wa haki za binadamu ni njia mojawapo ya kutatua migogoro hiyo. Chati Na. 36 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 36: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 36

Kwa upande mwingine, watahiniwa 117,790 (8.72%) waliochagua kipotoshi A, *Kuwa na jeshi moja hawakuwa sahihi kwa sababu jeshi moja lenye nguvu kwa maana ya kuunganisha nguvu za kijeshi Barani Afrika*, ni kuwa na nguvu kubwa ya kijeshi, askari waliopewa mafunzo ya hali ya juu na silaha za kisasa. Matumizi ya nguvu za kijeshi hayawezi kutatua migogoro hasa pale ambapo kuna ukiukwaji wa haki za binadamu. Pia, watahiniwa 114, 794 (8.50%) waliochagua kipotoshi B, *Kuondoa umaskini na utu hawakua sahihi kwani kipotoshi hiki kilihusisha kuondoa utu*. Utu ni hali ya kuwa na utambuzi wa utekelezaji wa wajibu kwa nafsi ya mtu na kwa jamii yake juu ya maisha; ni hali ya kuwa na tabia zinazolingana na hadhi ya mtu au ubinadamu. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa utu ukiondolewa ukandamizaji na unyonyaji

hupata nafasi na hii huchochea zaidi migogoro badala ya kuitatua. Hivyo, haiwezi kumalizwa ikiwa hakuna uadilifu.


Vilevile, watahiniwa 253,315 (18.75%) waliochagua kipotoshi C, *Kupambana na rushwa na uzalendo* hawakuwa sahihi kwa sababu kilihusisha dhana ya kupambana na uzalendo. Uzalendo ni kuwa na mapenzi na nchi yako na hata ikibidi kuipigania hadi kufa. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kuupinga uzalendo ni kukaribisha usaliti na utawala mbovu ambaao huchochea migogoro badala ya kuitatua. Pia, vita dhidi ya rushwa haviwezi kuzaa matunda bila uwepo wa uadilifu. Aidha, watahiniwa 223,208 (16.52%) waliochagua kipotoshi D, *Kuanzisha balozi katika nchi husika* hawakuwa sahihi kwani ubalozi ni ofisi ya uwakilishi wa nchi moja katika nchi nyingine ambayo hutoa huduma mbalimbali. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa kazi ya Balozi katika nchi ni kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi. Aidha, mahusiano baina ya nchi yanayoongozwa na sheria za kimataifa na sera ya mambo ya nje inayoongoza nchi husika, ambayo pamoja na mambo mengine inataka nchi kuheshimu haki ya nchi kujitawala na mipaka yake. Kwa hiyo, hatua ya kufungua ofisi za mabalozi bila kuambatana na hatua nyingine hakuwezi kumaliza migogoro.

Swali la 37: Tanzania ni nchi inayojulikana duniani kwa ukarimu na amani. Watanzania wanaishi kwa kufuata misingi ipi?

- A Umoja, upendo na mshikamano
- B Utulivu, ushirikiano na uadilifu
- C Uwazi, ustahimilivu na upendo
- D Umoja, uvumilivu na mshikamano
- E Upendo, ushirikiano na ujamaa

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kudumisha Amani* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu namna nchi ya Tanzania ilivyofanikiwa kujenga urafiki mwema na mataifa mengine. Swali

lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 957,738 (70.90%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 393,055 (29.10%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Umoja, upendo na mshikamano* walielewa tunu mbalimbali za taifa. Tanzania kwa miaka mingi imekuwa kisiwa cha amani na limekuwa kimbilio la wakimbizi wengi kutoka katika nchi zilizokumbwa na migogoro na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Pia, Tanzania ilitoa misaada ya hali na mali katika kipindi cha ukombozi wa nchi za Afrika. Aidha, Tanzania ilikuwa makao makuu ya vyama vilivyokuwa vinapigania uhuru wa nchi zao hasa za Kusini mwa Afrika. Tunu nyine ni utu, uzalendo na amani. Chati Na. 37 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 37: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 37

Kwa upande mwingine, watahiniwa 86,280 (6.39%) waliochagua kipotoshi B, *Utulivu, ushirikiano na Uadilifu* hawakutambua kuwa utulivu ni hali ya kuishi sehemu yenye upendo, ulinzi na amani. Pia, ushirikiano ni hali ya kufanya kazi pamoja kwa ajili ya kutimiza lengo moja na uadilifu ni sifa ya mtu mkweli na mwaminifu. Ushirikiano na uadilifu ni matokeo ya kuheshimu tunu za taifa. Utulivu, ushirikiano na uadilifu siyo tunu za taifa, bali ni matokeo ya tunu za taifa. Aidha, watahiniwa 78,344 (5.80%) waliochagua C, *Uwazi, ustahimilivu*

na upendo hawakuwa sahihi kwa kuwa chaguo hili lilihusisha uwazi na ustahimilivu. Uwazi ni hali ya serikali kuweka taarifa zake wazi kwa ajili ya wananchi na kuwa tayari kupokea maoni wakati ustahimilivu ni hali ya mtu kuweza kuchukua mambo mazito na kuyakabili bila kulalamika. Uwazi na ustahilivu ni matokeo ya kuishi kwa kufuata misingi ya tunu za taifa.


Vilevile, watahiniwa 119,771 (8.87%) waliochagua kipotoshi D, *Umoja, uvumilivu na mshikamano* hawakuwa sahihi kwa kuwa chaguo hili lilihusisha uvumilivu ambacho ni kitendo cha mtu kuwa na subira, kuwaelewa na kuwavumilia watu ambao una tofauti nao kwa namna tofauti tofauti. Uvumilivu ni matokeo ya upendo; watu wakipendana huvumiliana. Mwisho, watahiniwa 94,969 (7.03%) waliochagua kipotoshi E, *Upendo, ushirikiano na Ujamaa* pia hawakuwa sahihi kwani Ujamaa ni mfumo wa kiuchumi na kisiasa wenyewe kusisitiza ushirika katika kumiliki mali ya asilii dhidi ya umiliki binafsi.

Swali la 38: Ni njia ipi inaweza kutumika ili kuepukana na athari zitokanazo na utandawazi katika jamii?

- A Kuhamasisha maendeleo ya sayansi na teknolojia
- B Kutoa elimu kuhusu madhara ya utandawazi
- C Kulinda maudhui ya vyombo vyahabari vyakimataifa
- D Kutumia mitaala ya kimataifa katika kujifunza
- E Kuiga ustaarabu na utamaduni wa nchi za kigeni

Swali lilitungwa kutoka katika umahiri wa *Kudumisha Amani* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutathmini athari za utandawazi katika jamii. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 847,598 (62.75%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 503,195(37.25%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliobaini jibu sahihi B; *Kutoa elimu kuhusu madhara ya utandawazi* walielewa kuwa utandawazi ni mfumo wa uhusiano wa kimataifa katika nyanja mbalimbali

kama biashara, uchumi, siasa, jamii na utamaduni. Pia, walifahamu kuwa Tanzania hunufaika na utandawazi kutokana na kuongezeka kwa nafasi za ajira, uwekezaji, kupungua kwa vikwazo vyta kiuchumi, maendeleo ya teknolojia, kupanuka kwa soko la ndani na nje na maendeleo ya kijamii. Pamoja na hayo, watahiniwa walifahamu kuwa madhara ya utandawazi kama kuongezeka kwa mmomonyoko wa maadili, kuua viwanda vyta ndani, kufa au kudumaa kwa viwanda vyta ndani, kuathiri uhuru wa nchi kufanya maamuzi yake bila kuingiliwa, kuongezeka kwa uhalifu wa kimtandao, ugaidi na kukithiri kwa unyonywaji kiuchumi kwa nchi zinazoendelea. Chati Na. 38 inaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.



Chati Na. 38: Ufaulu wa watahiniwa katika swalii la 38

Hata hivyo, watahiniwa 189,390 (14.02%) walichagua vipotoshi A, *Kuhamasisha maendeleo ya sayansi na teknolojia*, 145,912 (10.80%) C, *Kulinda maudhui ya vyombo vyta habari vyta kimataifa*, watahiniwa 78,233 (5.79%) walichagua kipotoshi D, *Kutumia mitaala ya kimataifa katika kujifunza na watahiniwa* 74,491 (5.51%) walichagua kipotoshi E, *Kuiga ustaarabu na utamaduni wa nchi za kigeni*. Machaguo haya hayakuwa sahihi kwa sababu yalihusiana na matokeo hasi na chanya ya utandawazi na siyo njia za kuepusha athari hizo. Kwa mfano chaguo A, *Kuhamasisha maendeleo ya sayansi na teknolojia* uhaulishaji wa teknolojia kwa njia mbalimbali kama uwekezaji

kwenye tafiti za kisayansi, uwekezaji kiuchumi kutoka nje na kupanuka kwa soko la ajira kuliko sababisha wataalam wa teknolojia kutafuta ajira nchini. Pia, chaguo C, *Kulinda maudhui ya vyombo vya habari vya kimataifa* lilikuwa ni matokeo ya kuenea kwa makampuni makubwa ya habari duniani kama vile British Broadcasting Cooperation (BBC), Cable News Network (CNN) na Aljazeera kwa kutumia kivuli cha hati miliki, makampuni haya hulinda maudhui ya vyombo vyao.


Vilevile. Watahiniwa waliochagua kipotoshi D, *Kutumia mitaala ya kimataifa* hawakuelewa kuwa lilihusiana na kupanuka kwa wigo wa upatikanaji wa elimu ambao ulichochewa na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Hii imeondoa mipaka ya upatikanaji elimu kwani mitaala ya kimataifa imepata ushawishi mkubwa sehemu mbalimbali duniani. Mfano mzuri ni uwepo wa shule za kimataifa na zinazo tumia mtaala wa Cambridge hapa nchini pamoja na vyuo vya nje vinavyotumia elimu kwa njia ya mtandao.

Vilevile, chaguo E, *Kuiga ustaarabu na utamaduni wa nchi za kigeni* lilihusiana na kutokuwepo kwa mipaka ya kiutamaduni ambapo utamaduni na ustaarabu wa kimagharibi husambaa kwa njia mbalimbali kama kupitia elimu, vyombo vya habari, uhamaji wa watu, bidhaa kutoka nje na teknolojia. Matokeo yake ni watu hasa vijana kuiga baadhi ya mila na desturi za kimagharibi kama mavazi na mitindo mbalimbali ya kimaisha. Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika kipengele hiki unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakufahamu njia anuai za kuzuia athari za utandawazi katika jamii. Baadhi ya njia zinazoweza kutumika kukabiliana na utandawazi ni kama kuboresha elimu ili kuendana na mahitaji yaliyopo, kuhamasisha uzalishaji na kulinda viwanda vya ndani, kutunga na kusimamia sheria za kulinda mazingira na tamaduni zetu, kuwajengea uwezo wawekezaji wa ndani na kuijunga na jumuiya za kikanda ili kuwa na sauti ya pamoja katika kutetea maslahi yetu.

Swali la 39: Tanzania inafaidikaje kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

- A Kufanya biashara na mataifa wanachama
- B Kupanua soko la bidhaa zinazoagizwa kutoka nje
- C Kuingiliana kwa tamaduni za kigeni
- D Kupanua ufadhibili wa elimu ya juu
- E Kutumia bandari na mataifa nengine

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kudumisha Amani* na lilitaka mtahiniwa kubaini faida ambayo Tanzania inaipata kwa kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 na uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 524,473 (38.83%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 826,320 (61.17%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa walioweza kubaini jibu sahihi A, *Kufanya biashara na mataifa wanachama* walikuwa na uelewa juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa ni ushirikiano wa kikanda wa nchi saba ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, watahiniwa hao walielewa kuwa shughuli za kibiashara zinazofanyika kati ya Tanzania na nchi wanachama wa jumuiya hiyo huinufaisha Tanzania kiuchumi. Baadhi ya shughuli hizo zinahusisha sekta za kilimo na mifugo. Chati Na. 39 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




Chati Na. 39: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 39

Kwa upande mwingine, watahiniwa 398,854 (29.53%) waliochagua kipotoshi B, *Kupanua soko la bidhaa zinazoingizwa kutoka nje* hawakuwa sahihi kwa sababu kupanua soko la bidhaa kutoka nje ni kuruhusu uingizwaji zaidi wa bidhaa ambazo ni sawa na zile zinazozalishwa hapa nchini na hivyo kuuwa viwanda vyetu nya ndani. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa upanuaji wa soko la bidhaa kutoka nje hukwamisha ukuaji wa uchumi wa nchi kama hakutakuwa na utaratibu maalumu wa uingizaji bidhaa hizo. Pia, watahiniwa 129,600 (9.59%) waliochagua kipotoshi C, *Kuingiliana kwa tamaduni za kigeni* hawakuwa sahihi kwani msukumo mkubwa wa sera ya mambo ya nje ya Tanzania ni diplomasia ya uchumi, kwa hiyo uanachama wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ueleweke katika muktadha wa ushirikiano wa kiuchumi.

Vilevile, watahiniwa 196,191 (14.52%) waliochagua kipotoshi D, *Kupanua ufadhili wa elimu ya juu* hawakuwa sahihi kwani kupanua ufadhili wa elimu ya juu ni kitendo cha kuongeza fedha katika kuboresha na kuongeza kiwango cha utoaji wa elimu ya vyuo nya kati na vyuo vikuu. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kupanua ufadhili wa elimu ya juu hulenga zaidi mipango/manufaa ndani ya nchi binafsi/moja. Hata hivyo, nchi wanachama wana ushirikiano katika maeneo machache, hususani program za kubadilishana wanafunzi. Aidha, watahiniwa 86,121 (6.38%) waliochagua kipotoshi E, *Kutumia bandari na mataifa wanachama* hawakuelewa kuwa matumizi ya bandari ni sehemu ya kufanya biashara na nchi wanachama ambazo hazina bandari. Kwa hiyo bandari za Tanzania kutumiwa na nchi wanachama ni jambo lisiloepukika kutokana na hali hiyo chaguo tajwa halina uzito wa kustahili kuwa jibu sahihi. Mwisho, Tanzania ina bandari zake kwa ajili ya kuingizia bidhaa kutoka nchi za ughaibuni.

- Swali la 40:** Udumishaji wa amani unahusisha uwezo wa wanajamii katika kuchangamana. Ni kwa namna gani watu wenyewe tamaduni na asili tofauti wanaweza kuchangamana katika jamii?
- A Kwa kuheshimu tamaduni tofauti
 - B Kwa kubadilishana tamaduni zao
 - C Kwa kushirikiana wakati wa matatizo
 - D Kudumisha mila na desturi
 - E Kwa kubadilishana uraia

Swali hili lilitoka katika umahili wa *Kudumisha Amani*. Katika swalii hili, watahiniwa walitakiwa kubainisha njia inayoweza kutumiwa na watu wenyewe tamaduni na asili tofauti katika kuchangamana. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 617,635 (45.72%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 733,158 (54.28%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kwa kuheshimu tamaduni tofauti* walielewa kuwa kuheshimu watu wenyewe tamaduni na asili tofauti ni uwezo wa kuishi kwa kuwakubali watu hao na kuishi nao kwa amani na utulivu bila kujali tofauti hizo. Mahusiano mazuri hujenga kuaminiana, usalama na ustawi wa jamii na ndiyo mambo yanayojenga kuchangamana katika jamii. Chati Na. 40 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swalii hili.



Chati Na. 40: Ufaulu wa watahiniwa katika swalii la 40


Kwa upande mwingine, watahiniwa 101,487 (7.51%) waliochagua kipotoshi B, *Kwa kubadilishana tamaduni* zao hawakuwa sahihi kwa sababu ni hali ya watu wenye tamaduni na pengine historia tofauti kubadilishana mawazo, ujuzi, imani, mila na desturi. Kubadilishana utamaduni ni tukio linalochukua muda mrefu kutokea kwani ni matokeo ya watu hao kuishi pamoja kwa amani, furaha na kila mtu kuheshimu utamaduni wa mwenzake. Pia, watahiniwa 237,867 (17.61%) waliochagua kipotoshi C, *Kwa kushirikiana wakati wa matatizo* hawakuwa sahihi kwa sababu kushirikiana katika shida ni kitendo cha watu kukubaliana kwa hiyari yao kushirikiana katika kutatua changamoto zinazowakabili. Ushirikiano huu haulengi moja kwa moja katika kufanya watu wenye tamaduni na asili tofauti waweze kuchangamana katika jamii. Aidha, kushirikiana wakati wa matatizo hakuwezi kujenga hali ya kuchangamana katika jamii na huenda kusidumu endapo tatizo linalowaleta watu pamoja likapata ufumbuzi. Juhudi nyingine za ziada zinahitajika ili kujenga kuchangamana kwa watu wenye utamaduni tofauti.

Vilevile, watahiniwa 310,253 (22.97%) waliochagua kipotoshi D, *Kudumisha mila na desturi* hawakutambua kuwa kudumisha mila na desturi ni kuenzi matukio, mila na desturi za jamii fulani. Wakati mwingine kitendo cha kudumisha mila na desturi kinaweza kuleta mpasuko katika jamii kwa kundi moja lenye utamaduni tofauti kuona ni bora zaidi kuliko kundi jingine. Hali hii ilijidhihirisha wazi wakati wa utawala wa kibaguzi nchini Afrika Kusini. Mwisho, watahiniwa 68,063 (5.04%) waliochagua kipotoshi E, *Kwa kubadilishana uraia* hawakujua kuwa Tanzania ina taratibu za kisheria zinazotoa mwongozo wa namna ya kuomba uraia. Uraia wa Tanzania hautolewi kiholela kwa lengo la kuchangamana kwa jamii zenye utamaduni tofauti.

2.2. SEHEMU B: Maswali na Majibu Mafupi

Swali la 41: Taja majukumu muhimu mawili ya kiranja mkuu wa shule.

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *kuheshimu jamii* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu majukumu mbalimbali ya viongozi katika ngazi ya shule ya msingi, hususan majukumu ya kiranja mkuu wa shule. Swali lilijibwa na watahiniwa 1,350,793 na uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 1,193,965 (88.40%) walipata alama kuanzia 1 hadi 2 na watahiniwa 156,630 (11.60%) hawakujibu kwa usahihi kwa kuwa walipata alama 0. Chati Na. 41 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 41: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 41

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 785,808 (58.18%) walipata alama zote 2. Watahiniwa walitaja kwa usahihi majukumu mawili ya kiranja mkuu kama kuwa *msimamizi mkuu wa majukumu ya wanafunzi wote shulenii* na kuwa *mwenyekiti wa baraza la wanafunzi*. Pia, watahiniwa walielewa kuwa ni *msimamizi mkuu wa shughuli/majukumu ya wanafunzi* kama kufanya usafi wa mazingira ya shule na kusimamia sheria na taratibu za shule. Pia, huwa na jukumu la *usimamizi mkuu wa majukumu yote ya*

viranja katika vitengo vyao. Kadhalika, watahiniwa hao walielewa kuwa kiranja mkuu *ni kiunganishi kati ya walimu na wanafunzi*. Hufikisha *maswala/maoni ya wanafunzi kwa uongozi wa shule/utawala* na pia hufikisha *maagizo na maelekezo kutoka kwa uongozi*. Watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuwa walihawilisha mafunzo ya darasani na uhalisia. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubaini matakwa ya swali la 41.

SWALILA 41 *ijkiungo kati ya walimu na wanafunzi
ij kusimamia vikao yya wanafunzi*

Kielelezo Na. 1.1: *Ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi*

Katika Kielelezo 1.1. Mtahiniwa aliweza kutaja majukumu muhimu mawili ya kiranja mkuu wa shule kwa usahihi.

Aidha, watahiniwa 408,157 (30.22%) waliopata alama 1 walitaja jukumu moja tu la kiranja mkuu kwa usahihi kati ya mawili yaliyotakiwa katika swali hili. Watahiniwa wengine katika kundi hili walipata alama 1 kwa sababu walirudia hoja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu *kusimamia viranja wa chini waweze kusimamia kazi na kusimamia kazi ndogondogo*. Wapo watahiniwa waliochanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kuwasimamia viranja wenzake ambalo ni jukumu sahihi, kisha akaongeza kutoa mawazo*.

Changamoto nyingine ilijojitokeza ni kushindwa kutofautisha kati ya majukumu ya Mwalimu mkuu/uongozi wa shule na majukumu ya kiranja mkuu. Kwa mfano, watahiniwa wengine waliandika *kutunga sheria za shule na kuhakikisha vifaa vya kujifunzia vinapatikana shuleni* kama hoja ya kwanza, kisha

kusimamia usafi wa mazingira kama hoja ya pili hivyo kupata alama 1.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 156,630 (11.60%) waliopata alama 0 hawakuwa na maarifa ya kubaini muundo wa uongozi wa shule ikiwa ni pamoja na majukumu ya viranja/viongozi wa shule. Walishindwa kutafsiri matakwa ya swali na kuandika mambo yasiyo majibu sahihi. Mathalani, baadhi ya watahiniwa walitaja vyeo mbadala vyta kiranya mkuu kwa kuandika *kaka mkuu na dada mkuu* wakimaanisha majukumu ya kiranya mkuu. Hata hivyo, watahiniwa wengine walitaja sifa za kiongozi bora wa wanafunzi shulenii wakimaanisha majukumu ya kiranya mkuu kama vile *kutii sheria za shule, anaye wasiliana vizuri, kujua namna ya kuwaongoza wanafunzi wengine, kuwa na nidhamu, kuwa mwaminifu, kuwa muwazi, kuwa mwema kwa wengine, kuepuka tabia mbaya shulenii na kuwafundisha wengine tabia njema.*

Wanafunzi wengine kwa kukosa uelewa wa majukumu ya kiranya mkuu waliorodhesha majukumu ya viongozi wengine wa wanafunzi shulenii na wengine walichanganya na mambo yasio na uhusiano na swali waliloulizwa. Kwa mfano, waliandika *kuandika majina ya waongea Kiswahili, ufaulu wa kitaaluma wa wanafunzi na kufanya usafi.*

Vilevile, watahiniwa wengine walishindwa kutofautisha kati ya majukumu ya kiranya mkuu na mamlaka za uongozi wa shule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *nidhamu ya wanafunzi na heshima ya walimu wote*. Mtahiniwa huyo hakujua kuwa swala la nidhamu ya wanafunzi na heshima mionganii mwa walimu ni jukumu la uongozi wa shule na siyo la kiranya mkuu. Katika kundi hili, mtahiniwa mwingine alijibu *kuchagua wanafunzi wengine*; huyu hakuelewa kuwa kuchagua wanafunzi ni haki ya kila mwanafunzi katika shule husika. Pia, mtahiniwa mwingine aliandika *kutoa mawazo*. Mtahiniwa huyu pia alishindwa kuelewa kuwa kila mwanafunzi anaruhusiwa kutoa

mawazo kwa mwanafunzi mwenzake au uongozi wa shule kwa ajili ya maendeleo ya shule.

Vilevile, wapo watahiniwa walioeleza matendo ya kupenda shule na kuwasaidia walimu shughuli ndogondogo badala ya majukumu ya kiranya mkuu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja majukumu ya kiranya mkuu kuwa ni *kuimba wimbo wa shule* na *kuchota maji ya mwalimu*. Pia, watahiniwa wengine walieleza majukumu ya kila mmoja shulenii kama *jumuiya kuhakikisha ulinzi na usalama wa mazingira na mali za shule*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja *kulinda mazingira* na *kulinda rasilimali za shule* akimaanisha majukumu ya kiranya mkuu.

Changamoto nyingine iliyojitekeza ni kuwa baadhi ya watahiniwa kutokuwa na uelewa wa maudhui ya umahiri husika. Walinakili baadhi ya sentensi au vifungu vyaa maneno kutoka katika karatasi ya maswali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alinakili *Kudumisha mitazamo ya mafanikio* ambalo liliwa chaguo A katika swali la 26. Vilevile, mtahiniwa huyo alinakili *Kudumisha nidhamu ya darasa ambalo liliwa chaguo D* katika swali la 28. Mtahiniwa mwingine, alinakili *Usimamizi wa biashara* ambalo liliwa chaguo A katika swali la 20. Aidha, watahiniwa wengine walieleza njia mbalimbali za kumpata kiranya mkuu na msukumo wa kuchagua viongozi wa wanafunzi shulenii. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika *anateuliwa na wanafunzi shulenii, kutendeka kwa demokrasia na kuchagua kwa njia sahihi/nzuri*. Vielelezo Na. 1.2(a)-(b) ni sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili.

SWALI LA 41

Wimbo wa shule

Ntembo ya shule.

Kielelezo Na.1.2(a): Sampuli ya majibu ya Mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi

SWALI LA 41


Ukuhakikisha kuyamazisha darasa kukiwiana makelele
kukusanya madafari kwa wakati, k.t.

Kielelezo Na. 1.2(b): Sampuli ya majibu ya Mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi

Katika vielelezo 1.2(a) na (b) Watahiniwa walishindwa kutambua matakwa ya swali lilitowataka kutaja majukumu muhimu mawili ya kiranja mkuu wa shule badala yake walieleza vitu vinavyoitambulisha shule kama vile wimbo wa shule na nembo ya shule katika kielelezo 1.2 (a). Katika kielelezo 1.2(b) mtahiniwa alitaja majukumu ambayo yanaweza kufanywa na kiongozi wa darasa na siyo kiranja wa shule kama kutuliza kelele darasani.

Swali la 42: Moja ya shughuli za maendeleo ya jamii ni kushirikiana katika kutunza na kuboresha mazingira. Njia zippi mbili zinaweza kutumiwa na wanajamii katika kutunza na kuboresha mazingira?

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *kuithamini jamii* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu njia zinazotumika kutunza na kuboresha mazingira. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 1,090,020 (82.71%) walipata alama 1 hadi 2 na watahiniwa 260,575 (17.29%) hawakujibu kwa usahihi kwa kuwa walipata alama 0. Chati Na. 42 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 42: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 41

Uchambuzi wa ufaulu katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 734,966 (54.42%) walipata alama zote 2. Watahiniwa hawa waliweza kubainisha njia mbili zinazotumiwa na wanajamii katika kutunza na kuboresha mazingira. Watahiniwa hao walielewa kuwa *kupanda miti* ni muhimu kwani huzuia mmomonyoko wa udongo, husababisha ongezeko la mvua na hewa ya oksijeni ambayo ni muhimu kwa binadamu. Pia, walielewa kuwa *kutumia nishati mbadala* hupunguza matumizi ya nishati zisizo rafiki kwa mazingira kama mkaa na kuni ambazo huchangia katika uchafuzi wa mazingira na kutoweka kwa misitu.

Vilevile, watahiniwa hao walielewa kuwa *kuzingatia njia sahihi za kilimo* kama kilimo cha matuta, mzunguko wa mazao, mchanyato na ufgaji usio wa kuhamahama huzuia mmomonyoko wa udongo na hutunza rutuba ya udongo. Watahiniwa waliotaja *kuzingatia elimu ya mazingira*, walielewa kuwa elimu ya mazingira huongeza ufahamu kwa wanajamii juu ya umuhimu wa kutunza mazingira kwani baadhi ya matendo ya uharibifu wa mazingira hutokana na kukosa ufahamu huo. Watahiniwa hao walitambua kuwa *kuzuia ujenzi holela* ni jambo la msingi katika kutunza na kuboresha mazingira kwani hupelekeea mafanikio katika mipango miji ambayo husaidia mpangilio wa mifumo ya maji taka. Aidha, watahiniwa walielewa

kuwa *kuwashirikisha* wadau katika kufanya tathmini ya mazingira na *kuunda vikundi* vya *utunzaji* wa mazingira ni njia nyingine ya *utunzaji* na uboreshaji wa mazingira. Vilevile uhusishwaji wa wadau katika kufanya tathmini ya mazingira hupunguza matokeo hasi/yasiyotarajiwa. Mwisho, watahiniwa walielewa kuwa *ulegelezaji* husaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira kwani taka kama plastiki ambazo hazi meng'enyeki huchakatwa upya kwa kuzalisha bidhaa nyingine. Kielelezo Na. 2.1 Ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyweweza kubaini matakwa ya swali la 42.

SWALI LA 42

SF Kupanda miti

S3 Kuepuko kutilma karibu na vyanzo vya maji

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali la 42 kwa usahihi

Katika Kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa aliweza kutaja njia mbili zinazoweza kutumiwa na wanajamii katika kutunza na kuboresha mazingira.

Hata hivyo, watahiniwa 355,054 (26.29%) waliopata alama 1, walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine walishindwa kutoa idadi ya hoja zilizotakiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *mahitaji ya kuni na mkaa na kupanda miti* ambalo ni jibu sahihi. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa mahitaji ya kuni na mkaa hupelekea ukataji wa miti na hatimaye uharibifu wa mazingira. Mtahiniwa mwengine aliandika *kutunza vyanzo vya maji na kukata miti* ambalo siyo jibu sahihi kwani ukataji miti hupelekea ukame na kuenea kwa jangwa. Vilevile, mtahiniwa mwengine aliandika *kukata miti* ambalo siyo jibu sahihi na *kupanda miti* ambalo ni jibu sahihi.

Kwa upande mwengine, watahiniwa 260,575 (19.29%) walishindwa kueleza njia zinazoweza kutumika katika kutunza

na kuboresha mazingira, hivyo walipata O. Baadhi ya watahiniwa walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo walitaja vifaa vinavyotumika katika kuboresha mazingira, mfano mtahiniwa mmoja alitaja *kutumia majembe, kwanja na ufagio*. Pia, watahiniwa wengine walieleza shughuli mbalimbali za kibinadamu zinazopelekea uharibifu wa mazingira kama *kuchoma moto vichaka na majani, kuchoma misitu, kutupa taka hovyo, kujisaidia kwenye mito, kulima kandokando ya mito na kulima karibu na vyanzo vya maji*. Vilevile, watahiniwa wengine walieleza faida za kutunza mazingira, mfano *kuboresha mazingira kwa afya yako*.

Aidha, watahiniwa wengine waliainisha tabia ambazo wanajamii wanapaswa kuwa nazo katika shughuli za kutunza na kuboresha mazingira. Mathalani, *kuwa na ushirikiano na kujituma*. Mwingine alieleza madhara ya mahusiano mabaya katika jamii kama *kugombana na kunyanyasana*. Watahiniwa wengine walijikita katika kueleza vichocheo vya ustawi wa maendeleo ya jamii kama vile *ushirikiano wa jamii na amani katika jamii*. Vilevile, watahiniwa wengine waliandika umuhimu wa kuweka mazingira safi. Kwa mfano, *kufyeka na kulima nyasi na vichaka vilivyopo kandokando na makazi ili kuzuia mlipuko wa magonjwa na kuepuka wadudu hatari mfano nyoka*. Watahiniwa wengine walihusianisha njia za kutunza na kuboresha mazingira na kujitunza binafsi. Kwa mfano, *kujipenda na kujithamini*.

Aidha, watahiniwa wengine kwa kukosa uelewa wa njia zinazoweza kutumiwa na wanajamii katika kutunza na kuboresha mazingira, walinakili baadhi ya vifungu vya maneno na sentensi kutoka katika karatasi ya maswali. Kwa mfano, *usimamizi mzuri wa fedha ambalo ni chaguo C katika swali la 20*. Pia, mtahiniwa mwingine alinakili baadhi ya maneno kutoka katika maelekezo yaliyotolewa katika kujibu maswali ya sehemu B ya mtihani huu kwa kuandika *kalamu ya wino*. Mifano mingine ya watahiniwa ambao walinakili baadhi ya sehemu za maswali

ni kufanya kazi kwa pamoja, kushirikiana katika maendeleo na kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Vilevile, watahiniwa wengine walienda mbali kwa kuelezea mambo yasiyohusiana kabisa na kutunza na kuboresha mazingira. Kwa mfano, kushiriki katika michezo mbalimbali. Kielelezo Na. 2.2 Ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa swali hili.


SWALI LA 42	
I) Kutumia njia ya kilimo	
II) Kutumia njia tuliflizaji	

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi

Katika **Kielelezo Na. 2.2.** mtahiniwa hakuweza kubainisha njia zinazoweza kutumiwa na wanajamii katika kutunza na kuboresha mazingira badala yake alitaja shughuli za maendeleo hasa kijijini zinazoweza kuboresha maendeleo ya wanajamii.

Swali la 43: Mtokambali amekuwa na mazoea ya kukiuka sheria za usalama barabarani. Je madhara yapi mawili yanayoweza kumpata?

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *kuwa mwajibikaji* na liliwataka watahiniwa kubainisha madhara yanayoweza kumpata mtu kwa kutotii sheria na kanuni za usalama barabarani. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 na uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 1,172,349 (86.80%) walipata alama 1 hadi 2 na watahiniwa 178,246 (13.20%) hawakujibu kwa usahihi. Chati Na. 43 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 43.



Chati Na. 43: Ufaulu wa watahiniwa katika swalii la 43

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swalii hili ulionesha kuwa watahiniwa 425,869 (31.53%) walipata alama zote 2 katika swalii hili. Walibainisha kwa usahihi madhara ya kukiuka sheria za usalama barabarani. Madhara yaliyobainishwa ni pamoja na *kupata ajali zinazoweza kusababisha majeraha, vifo au ulemavu; faini na adhabu nyingine kama kifungo cha gerezani*. Pia, *kupoteza leseni; kugharimia matibabu; kuongeza msongamano barabarani na kusababisha hasira na hofu kwa watumiaji wengine wa barabara*. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa kwamba ajali hutokea endapo mtumiaji wa barabara atapuuza sheria za usalama barabarani. Pia, *ataendesha chombo cha moto kwa mwendokasi, kutokea kwa mabadiliko ya hali ya hewa, utumiaji wa pombe na dawa za kulevyta, miundombinu mibovu ya barabara na uchovu pamoja na kutofuata kanuni za afya na sheria za usalama*. Kielelezo Na. 3.1 Ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyweweza kubaini matakwa ya swalii la 43.

SWALI LA 43

Kifaa
Kupata ajali imayeweza kumsababishia majeraha

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya majibu kutoka kwa mtahiniwa aliyejibu swalii la 43 kwa usahihi

Katika Kielelezo Na. 3.1 Mtahiniwa aliweza kubaini madhara ambayo yanaweza kumpata mtu/Mtokambali kwa kukiuka sheria za usalama barabarani.

Hata hivyo, watahiniwa 746,480 (55.27%) waliopata alama 1 hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya madhara ya kukiuka sheria za usalama barabarani. Baadhi ya watahiniwa walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kugongwa na gari* ambalo ni jibu sahihi na *kutozingatia alama za barabarani* ambapo hoja hii ilihu sababu au vyanzo vya ajali. Mtahiniwa mwengine aliandika *kupata ajali* ambalo ni jibu sahihi na *anaweza kupata magonjwa* ambalo siyo jibu sahihi na mwengine aliandika *anaweza kupata ajali* ambalo ni jibu sahihi na *ujambazi wa watu*, jibu lisilo sahihi. Watahiniwa wengine waliandika hoja mbili zinazofanana kama majibu mawili yanayotofautiana. Kwa mfano, *kupata ajali* kama hoja ya kwanza na *kuwagonga watu wengine* kama hoja ya pili wakati zote zinarejea tukio la ajali.

Kwa upande mwengine, watahiniwa 178,246 (13.20%) waliopata 0, walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kutokuandika majibu sahihi juu ya madhara ya kutozingatia sheria za usalama barabarani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika mambo yaliyohusiana na kudumisha usafi na kanuni za utawala bora kama *utawala wa sheria na kuepuka magonjwa*. Pia, watahiniwa wengine walieleza adhabu ambazo hutolewa kwa wanaosababisha ajali mfano, *kudhibitiwa vikali na kulipa fidia*. Watahiniwa wengine waliandika matendo ambayo wanafanyiwa waliosababisha ajali kwa utaratibu usio rasmi/usio wa kawaida. Kwa mfano, *kukamatwa na kupigwa; hatapata pa kwenda na hatapata uaminifu*. Mwisho, kuna watahiniwa waliohusianisha neno madhara na maradhi au magonjwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kuumwa ugonjwa wa miguu na ugonjwa wa misuli na kupungua maji mwilini, kutokuwa vizuri katika viungo vyake*. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha mtahiniwa aliyetoea majibu yasiyo sahihi.

SWALI LA 43


i) Kuwa kuheshimu tamaduni tofauti
 ii) Kuwa kubaliana tamaduni zao

Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mtahiniwa katika swali la 43

Katika Kielelezo Na. 3.2. mtahiniwa hakuweza kutaja madhara ambayo yanaweza kumpata Mtokambali kwa kukiuka sheria za usalama barabarani badala yake alieleza mambo ya kuzingatia ili kuweza kuishi kwa amani na watu wa tamaduni tofauti.

Swali la 44: Rushwa ni miongoni mwa changamoto za maendeleo katika taifa. Ni tunu zipi mbili za taifa zinaweza kutumiwa katika kupambana na rushwa nchini Tanzania?

Swali lilitungwa kutoka katika umahiri wa *kuwa mwadilifu* na lilitaka mtahiniwa abainishe tunu mbili za taifa zinazoweza kutumika katika kupambana na rushwa nchini. Swali hili liliikuwa na ufaulu hafifu kuliko maswali yote katika mtihani huu. Swali lilijibowi na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 192,969 (14.29%) pekee walipata alama 1 hadi 2 na watahiniwa 1,157,626 (85.71%) walipata 0. Chati Na. 44 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 44: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 44

Watahiniwa 60,252 (4.46%) walipata alama 2 katika swali hili. Hawa walikuwa na ufahamu kuhusu njia za kuzuia na kupambana na rushwa nchini. Walibainisha tunu za taifa zinavyoweza kutumika kuzuia na kupambana na rushwa nchini ambazo ni *umoja, uadilifu, uzalendo, uwajibikaji, utu*, na *uwazi*. Watahiniwa waliotaja umoja walielewa kuwa katika kupambana na rushwa lazima kuwa na umoja unaoweza kusaidia kumaliza tatizo la rushwa. Baadhi ya watahiniwa walibaini tunu ya uadilifu wakimaanisha kufanya jambo lililojema na haki bila kupendelea upande wowote. Halikadharika, watahiniwa walioandika uzalendo walifahamu kuwa kuwepo na juhudhi ya kila mmoja katika kuipenda moyoni na kuitangaza nchi yetu kwa matendo. Tunu nyiningine ambayo ni muhimu katika mapambano dhidi ya rushwa ni uwazi ambao huimarisha utawala bora na kupunguza rushwa katika utendaji kazi, hasa katika mapato na matumizi. Tunu nyiningine ni uwajibikaji ambapo hujumuisha viongozi kuwa na uwezo wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa wafanyakazi, kutoa taarifa zenye ukweli na kwa wakati pia zinazoelewaka. Mwisho, watahiniwa waliobainisha uwepo wa utu walikuwa na uelewa kwamba kutanguliza utu katika matendo yetu kama binadamu, uungwana, kupenda haki, kauli njema na hekima husaidia kupunguza rushwa nchini. Kielelezo Na. 4.1 Ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.

SWALI LA 44	(i) UZALENDO (ii) UWAJIBIKAJI

Kielelezo na. 4.1: *Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 44*

Katika kielelezo 4.1. mtahiniwa aliandika tunu mbili mionganis mwa zinazoweza kutumika katika kupambana na rushwa nchini.

Halikadhalika, watahiniwa 132,717 (9.83%) walipata alama 1 walionesha uelewa wa wastani juu ya tunu za taifa na namna zinavyoweza kutumika katika kupambana na rushwa nchini. Waliandika majibu mchanganyiko: ambayo ni sahihi na ambayo siyo sahihi. Kwa mfano; *uchaguzi wa huru na haki, uhuru wa nchi kujitawala na utawala wa sheria*. Majibu haya hayakuwa tunu za taifa, bali yalihusiana na misingi ya demokrasia na utawala bora. Uhuru wa nchi kujitawala ni moja ya sifa kuu ya taifa lolote huru kwani ni hali ya taifa fulani kufanya maamuzi yake bila kuingiliwa na mataifa au mamlaka nyingine kutoka nije ya nchi. Pia uchaguzi huru na haki ni sehemu ya misingi ya demokrasia ya uwakilishi ambayo huwapa wananchi fursa ya kuchagua kiongozi wanayetaka awaongoze au awawakilishe, kadharika utawala wa sheria ni utawala unaotekeleza sheria kwa watu wote kwa usawa.

Mifano mingine ya majibu ambayo hayakuwa sahihi ni *busara, upendo na utilivu*, ambazo ni sifa binafsi za mtu aliyestaarabika. Wengine walitaja vyombo vinavyohusika na kupambana na rushwa kama vile *PCCB na Polisi*. Hata hivyo, kuna watahiniwa waliotaja tunu moja tu badala ya mbili kama swali lilivyowataka; hii ilisababisha watahiwa hawa kupata nusu ya alama kati ya 2. Kwa mfano “*umoja*” na ndio lilikuwa jibu lake pekee katika swali hili.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,157,626 (85.71%) walipata alama 0. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili umebaini udhaifu ulisababishwa na watahiniwa kukosa uelewa juu ya tunu na namna zinavyoweza kutumika kupambana na rushwa. Wengine hawakuelewa matakwa ya maswali. Kwa mfano, waliandika taasisi mbalimbali za kupambana na rushwa, taasisi za kimataifa, vyombo vya ulinzi na usalama, alama za taifa na vyeo vya makamanda wa police. Mfano wa majibu hayo ni kama vile, *TAKUKURU, JWTZ, UNESCO, IGP, Jeshi la Polisi, Mwenge na Serikali*.

Vilevile, watahiwa wengine walishindwa kutofautisha kati ya tunu za taifa na mihimili mitatu ya nchi ambayo ni *Mahakama, Bunge na Serikali*. Hawakujua kwamba kazi ya mahakama ni kutafsiri sheria na kutoa haki, kazi ya bunge ni kutunga sheria na kazi ya serikali ni kutekeleza sera na sheria zilizotungwa na Bunge. Aidha, baadhi ya watahiniwa waliandika ushauri wa hatua za kuchukua ili kupambana na rushwa badala ya tunu za taifa. Mfano waliandika *kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi, kutoa elimu juu ya madhara ya rushwa, kuchukulia sheria wala rushwa, kutumia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, kutumia Asasi za Kiraia, kusimamia haki za binadamu, kujilinda na kulinda wengine na kutoa huduma za kijamii*. Watahiniwa wengine walikwenda mbali zaidi kwa kuandika *kupendekeza kuwe na midahalo, mtu akiona matukio ya rushwa apige simu 113, kupiga simu polisi na kutoa taarifa TAKUKURU*. Majibu haya yasiyo sahihi yanaonesha kuwa watahiniwa hawakujua tunu za taifa na wajibu wa kupambana na rushwa nchini.

Licha ya hao, kuna watahiniwa waliotaja aina za rushwa kinyume na matakwa ya swali. Kama vile; *rushwa kubwa na rushwa ndogo*. Katika kundi hili, kuna watahiniwa waliotaja mambo kadhaa yanayoweza kuchochea vitendo vyta kutoa na kupokea rushwa. Kwa mfano, *umasikini, ukosefu wa elimu na ukosefu wa huduma za kijamii* kwa maana kwamba watu hupokea rushwa ili kuongeza kipato cha kujikimu, wengine hutoa rushwa kwa sababu ya kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya rushwa na haki zao, na wengine hutoa rushwa ili wapate huduma za kijamii. Zaidi ya yote, kuna watahiniwa waliokosa maarifa katika maudhui yaliyotahiniwa kiasi kwamba waliamua kunakili sentensi kutoka katika machaguo ya mtihani huu na kuyaweka kwenye majibu ya swali yawe kama tunu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alinakili chaguo B na E kutoka swali la 38; *Kutoa elimu kuhusu madhara ya utandawazi na Kuiga ustaarabu na utamaduni wa nchi za kigeni* na wapo watahiniwa ambao hawakujibu hili swali kabisa. Vielelezo na. 4.2(a)-(c) vinaonesha watahiniwa waliota majibu yasiyo sahihi.

SWALI LA 44

Q) TAKUKUZA

bivongoi wadini au madhehebu wa dini

**Kielelezo Na. 4.2(a): Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi
Kutoka kwa mmoja wa watahiniwa**

SWALI LA 44

1) TAKUKUZA na
2) TAKUSHI

**Kielelezo Na. 4.2(b): Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi
Kutoka kwa mmoja wa watahiniwa**

SWALI LA 44


Rushwa na Ngono Kutoka ngoro zembe

**Kielelezo Na. 4.2(c): Sampuli ya majibu yasiyo Sahihi
kutoka kwa mmoja wa watahiniwa**

Katika vielelezo Na. 4.2(a-c) Watahiniwa hawakuweza kubainisha tunu za taifa zinazoweza kutumiwa katika kupambana na rushwa nchini Tanzania badala yake waliandika mambo mengine ambayo hayahusiani na tunu za taifa.

Swali la 45: Ni njia zipi zinaweza kutumika kuboresha urafiki kati ya Tanzania na nchi nyingine? Bainisha njia mbili.

Swali hili lilitoka katika umahiri wa *Kudumisha Amani* na lilipima uelewa wa watahiniwa juu ya uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,350,793 ambapo watahiniwa 1,041,639 (77.13%) walipata alama kuanzia 1 hadi 2 na watahiniwa 308,956 (22.87%) walipata alama 0. Chati Na. 45, inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 45: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 45

Watahiniwa 694,409 (51.42%) wwalipata alama 2 walikuwa na ufahamu juu ya njia zinazoweza kutumiwa na Tanzania kuboresha mahusiano yake na nchi nyingine. Walibainisha njia hizo kuwa ni *kushiriki katika kutatua migogoro ya nchi nyingine, kujifunza utamaduni, siasa na uchumi wa nchi nyingine, kuonesha ukarimu kwa watu wa mataifa mengine, kutoa ushirikiano katika matumizi ya miundombinu na kuwa mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kimataifa*. Watahiniwa walioandika kuhusu Tanzania kushiriki katika utatuzi wa migogoro ya nchi nyingine walikuwa na uelewa kuwa Sera ya Tanzania ya Mambo ya Nje pamoja na mambo mengine inazingatia amani, usawa na utu. Hii ni kwasababu Tanzania ni nchi ya amani, imekuwa mwenyeji wa mazungumzo kwa nchi

mbalimbali zinazokumbwa na migogoro. Kwa mfano; Tanzania imekuwa mwenyeji wa mazungumzo na makubaliano ya amani katika migogoro ya Rwanda na Burundi kati ya mwaka 1993 na 2006 mjini Arusha ambayo yalisaidia wakimbizi kurudi kwao. Hivyo, Tanzania kupunguza changamoto zilizokuwa zinasababishwa na uwepo wa wakimbizi hao. Pia, Tanzania kwa kuititia viongozi wake, imekuwa kiungo muhimu katika kuleta utulivu wa kisiasa katika nchi mbalimbali. Kwa mfano, Rais mstaafu, Mh. Kikwete alikuwa kiongozi katika kusuluhisha mgogoro mwaka 2008 baina ya Mwai Kibaki na Raila Odinga uliotokana na uchaguzi. Kadharika, hayati Mkapa alikuwa msuluhishi wa mgogoro wa kikatiba ulioikumba Burundi mwaka 2018. Pia, Tanzania hushiriki katika ulinzi wa amani kwa kupeleka vikosi vya Jeshi katika mataifa mbalimbali, kama vile: Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Sudan Kusini, Msumbiji na Lebanon.

Aidha, watahiniwa walioandika *kujifunza utamaduni, siasa na uchumi wa nchi nyininge* walikuwa na uelewa kwamba Tanzania inajifunza tamaduni za nchi mbalimbali kama nyenzo ya kuimarisha mahusiano na nchi hizo. Kwa mfano, lugha kama Kichina, Kiarabu na Kifaransa zipo katika mtaala. Pia, Chuo Kikuu cha Dodoma kuna Taasisi ya Confucius ambayo ni maalumu kwa ajili ya kufundishia Lugha na Tamaduni za Jamhuri ya Watu wa China na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa upande wa michezo, Tanzania imekuwa ikishiriki mashindano mbalimbali kama vile ya Olimpiki na CECAFA. Kwa upande wa kisiasa, nchi yetu imekuwa ikikaribisha wangalizi wa uchaguzi kutoka nje, lakini pia viongozi wetu wamekuwa wakiaminiwa na kupewa nafasi ya kuongoza timu za waangalizi wa chaguzi katika nchi mbalimbali. Kwa mfano, Mh Jakaya Kikwete alikuwa kiongozi wa timu ya waangalizi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika uchaguzi mkuu wa Kenya mwaka 2022. Na kwa upande wa kiuchumi, Tanzania imekuwa ikichukua hatua muhimu kukaribisha watalii na wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali kuja kuwekeza Tanzania.

Vilevile, watahiniwa waliotaja *kuonesha ukarimu kwa watu wa mataifa mengine* walikuwa na uelewa kwamba watanzania ni maarufu kwa ukarimu hasa katika kuwajali wageni. Lakini pia, serikali ya Tanzania imekuwa ikipokea wakimbizi waliokimbia matatizo katika nchi zao na kuwapa hifadhi. Kwa mfano, Tanzania imekuwa makao makuu ya vyama vingi vya ukombozi wakati wa wapigania uhuru wa ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. Walionusurika katika mgogoro kati ya Wahutu na Watusi nchini Rwanda na Burundi walipata hifadhi nchini Tanzania. Waliotaja *kutoa ushirikiano katika matumizi ya miundombinu* nao wako katika kundi hili kwani walikuwa na uelewa kwamba Tanzania inashirikiana sana na nchi nyingine katika kuanzisha na kutumia miundombinu mbalimbali hasa ile ya kimkakati kama barabara, reli, bandari na nishati. Baadhi ya miradi hiyo ni mradi wa kufua umeme kwa maji Rusumo unaotekelezwa kati ya Tanzania na Rwanda. Kadhalika, Tanzania inashirikiana na Uganda kutekeleza mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi (The East African Crude Oil Pipeline). Miradi mingine ambayo ilishatekelezwa na Tanzania kwa utaratibu huo ni pamoja na Reli ya Tanzania kwenda Zambia (TAZARA), daraja la Umoja linalounganisha Tanzania na Msumbiji pamoja na bomba la mafuta ghafi linalotoka Tanzania kwenda Zambia (TAZAMA).

Mwisho, baadhi ya watahiniwa walibainisha hoja ya *Tanzania kuwa mwanachama wa Jumuiya mbalimbali za kimataifa*. Hawa walikuwa na maarifa juu ya Tanzania kuwa muasisi wa wazo la kuanzisha Jumuiya ya Umoja wa Afrika (OAU) mwaka 1963, baadae kuwa Umoja wa Afrika (AU) mwaka 2002. Pia, Tanzania ni muasisi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) mwaka 1992, na mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Masharika (EAC) mwaka 1967, na baadae mwaka 2000 na. Mpaka sasa, Tanzania ni mwanachama hai wa jumuiya zote hizo. Kadhalika, Tanzania ni mwanachama hai wa Jumuiya ya Madola na Umoja wa Mataifa. Kielelezo Na. 5.1 *ni sampuli ya majibu sahihi* ya mtahiniwa katika swali la 45.

SWALI LA 45

Tanzania kuna mwana dhama wa nchi zingine
kushirikiana katika biashara na shughuli zingine
za kudumi.

Kielelezo Na. 5.1: *Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 45*

Katika kielelezo 5.1 mtahiniwa alitaja kwa usahihi njia zinazoweza kutumika katika kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 347,230 (25.71%) waliopata alama 1 hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya njia za kudumisha uhusiano na mataifa mengine. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wengi katika kundi hili waliweza kuandika njia moja sahihi, ikifuatiwa na nyingine ambayo haikuwa sahihi na wachache walitoa jibu moja tu kati ya mawili yaliyotakiwa ili kujibu swali. Mifano watahiniwa waliopata jibu moja, na kuandika nyingine ambayo siyo sahihi. *njia za kufanya uhalifu*, wakati ni kitendo kinachowenza kuharibu kabisa uhusiano wa nchi hizo. Mwingine aliandika *kupanua soko la bidhaa zinazotoka nje*. Mwingine aliandika kauli mbiu ya taifa “*uhuru na umoja*”, hakujua kuwa uhuru na umoja hutumika kueleza malengo na nia ya taifa la Tanzania.

Pia, watahiniwa 308,956 (22.88%) waliopata 0 walionesha kutoelewa matakwa ya swali na wengine walishindwa kudhihirisha umahiri uliopimwa katika swali hili. Wapo waliohusianisha njia zinazotumika katika kuboresha urafiki kati ya Tanzania na nchi nyingine kwa upande mmoja na faida zinazotokana na mahusiano hayo kwa upande mwingine. Kwa mfano, *kupokea mikopo na kuimarisha ulinzi na usalama kupokea misaada ya fedha kutoka mataifa mengine na kupokea*

mikopo kupata fursa za kibiashara na kupata mikopo ya riba nafuu.

Sambamba na hao, wengine walihuisha njia za kutumika kuboresha urafiki kati ya Tanzania na nchi nyingine na utekelezaji wa tunu za taifa; mfano, *amani na mshikamano, upendo, umoja, kuthamini utu wa watu wengine, kujivunia nchi na kupenda nchi yako, kuwa mzalendo na kusema ukweli, kutotoa rushwa katika jamii, uwazi na uadilifu*. Watahiniwa wengine waliongeza namna bora ya kudumisha umoja katika nchi; mfano *kutokuchagua rangi, sura, dini kabila na kuthaminiana bila kunyanyasana*.

Watahiniwa wengine walipendekeza njia za kawaida ambazo zinatumika kuanzisha na kujenga uhusiano wa kawaida na siyo kidiplomasia. Kwa mfano, *kupata mawasiliano na kuwasiliana, kutumia mitandao ya kijamii, kuwa na tabia njema, kuwa msafi, kupata marafiki wema na kusoma shule moja, kutambulishana kwa mavazi, kutambulishana kwa lugha na kuitisha vikao*. Watahiniwa wengine walikwenda mbali zaidi na kueleza mambo yanayoweza kuimarisha mahusiano ya watu kama vile *kuongea na mwenzake, msigombane na rafiki yako, kudumisha upendo, kushirikiana katika shida na raha, kuwa mtu mwenye busara, kuwa mwelevu na kujiheshimu, kuwa mkweli na mwaminifu, kutoa misaada mbalimbali, kutoa misaada kwa yatima, na Kumwambia mtu maneno ya ukweli na kutomwambia mtu unafiki*.

Vilevile, baadhi ya watahiniwa waliohusianisha uboreshaji wa urafiki kati ya Tanzania na nchi nyingine na vyombo vya usafirisahaji vinavyotumika kusafirisha watu au bidhaa kutoka taifa moja kwenda lingine, kwa mfano *ndege za angani na meli*. Mwingine pia alitaja *usafiri wa anga na majini*. Vilevile, kuna watahiniwa waliohusianisha njia zinazoweza kutumika kuboresha urafiki kati ya Tanzania na nchi nyingine, kwa mfano, uundwaji wa mashirika ya kimataifa. Mfano *Tanzania kujiunga*

na FAO na UNO, na mwingine aliandika kuunda umoja wa mataifa. Mtahiniwa huyu alishindwa kutofautisha kati ya Tanzania kuwa mwanachama wa jumuiya mbalimbali na kuundwa kwa umoja wa mataifa, mwaka 1945.

Aidha, kuna watahiniwa waliohusianisha njia zinazoweza kutumika kuboresha urafiki kati ya Tanzania na nchi nyingine na maendeleo mbalimbali ya kisiasa katika nchi ya Tanzania. Kwa mfano; walitaja ASP na TANU kama vyama vya siasa vilivyopigania uhuru jambo ambalo siyo mionganoni mwa njia za kuboresha uhusiano kati ya Tanzania na nchi nyingine.

Mwisho, baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walinakili baadhi ya sehemu za maswali ya mtihani huu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alinakili *kusikiliza redio na kujisomea vitabu na kuangalia runinga na sinema* ambayo ni machaguo A na B ya swali la 29. Mtahiniwa mwingine alinakili *kubadilishana uraia* ambalo ni chaguo E la swali la 40. Kielelezo na. 5.2 kinaonesha mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyo sahihi.

SWALI LA 45

*Kupata Marufiki Wemla
Kutisoma Shule mja*

Kielelez Na. 5.2: *Sampuli ya Majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa katika swali la 45*

Katika kielelezo na.5.2, mtahiniwa aliandika hoja ambazo haziendani na hitaji la swali.

3.0 HITIMISHO

Takwimu za uchambuzi zinaonesha kuwa wastani wa ufaulu wa mahiri sita (6) zilizotahiniwa ulikuwa asilimia 56.31 ambao ni ufaulu wa wastani. Mtihani wa Uraia na Maadili wa mwaka 2022 ulipima mahiri sita (6) ambazo ni *kuheshimu jamii, kuitithamini*

jamii, kuwa mwajibikaji, kuwa mstahimilivu, kuwa mwadilifu na kudumisha amani.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa walipata ufaulu mzuri katika aina mbili za umahiri ambazo ni *kuithamini jamii* (68.40%) na *kuwa mwajibikaji* (64.33%). Umahiri uliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu ni *kuheshimu jamii* (53.77%) *kudumisha amani* 51.96%), *kuwa mwadilifu* (50.45%) na *kuwa mstahimilivu* (49.00 %).

Kwa ujumla, ufaulu wa umahiri wa watahiniwa ulikuwa wa wastani kwa mwaka 2021 na 2022 kwa kuwa ulikuwa na asilimia 51.2 na 56.31 mtawalia. Aidha, ulinganifu wa ufaulu wa umahiri uliotahiniwa katika Mtihani huu wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) kwa mwaka 2021 na 2022 unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu cha umahiri wa *Kuithamini Jamii* na *Kuwa Mwajibikaji* kilikuwa kizuri. Kuithamini Jamii wastani wa (62.90%) kwa mwaka 2021 na wastani wa (68.40%) katika mwaka 2022. Sawa na wa kuwa Mwajibikaji ufaulu wastani wa (60.8%) kwa mwaka 2021 na wastani wa (64.33%) mwaka 2022. Umahiri wa *Kuheshimu Jamii* ufaulu umeendelea kuwa wa wastani (50.10%) katika mwaka 2021 na (53.77%) katika mwaka 2022. Pia, ufaulu katika aina nyingine za umahiri ulikuwa na kiwango cha wastani kama ifuatavyo: *Kuwa Mwadilifu* ufaulu ulikuwa wastani wa (46.3%) mwaka 2021 na mwaka 2022 ulikuwa (50.45%). Ufaulu wa Kudumisha Amani ulikuwa 45.90 mwaka 2021 na mwaka 2022 ulikuwa wastani wa (51.96%), mwisho ufaulu wa umahiri wa Kuwa Mstahimilivu ulikuwa na ufaulu wa wastani (41.20%) kwa mwaka 2021 sawa na mwaka 2022 kwa wastani wa (49.00%).

4.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika aina za umahiri uliotahiniwa na ambao ulikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu yafuatayo yanapendekezwa kuzingatiwa:

- (a) Walimu washirikiane na wanafunzi katika kufundisha na kujifunza umahiri wa *kuheshimu jamii* na *kudumisha amani* kwa kusoma matini mbalimbali, magazeti, kusikiliza radio,

kuangalia runinga. Vyanzo hivi vya taarifa vitawawezesha wanafunzi kupata taarifa juu ya masuala mtambuka na masuala ya uhusiano wa kimataifa. Masuala mtambuka ni kama vile: mazingira, jinsia, haki za watoto, madawa ya kulevyta, demokrasia, utawala bora na haki za binadamu). Pia masuala ya uhusiano wa kimaifa ni kama vile; kudumisha biashara, michezo, sera za ushirikiano wa kimataifa na uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine.

- (b) Katika kufundisha kuhusu namna ya kubaini matakwa ya maswali, katika mahiri zilizotahiniwa, walimu wanashauriwa kutumia njia ya majadiliano katika vikundi vidogo, kutumia vielelezo vinavyoonesha maneno yenye ufunguo (key words), na chati yenye orodha ya maneno yanayoweza kutumika katika kuuliza maswali. Njia hii itawawezesha wanafunzi kuwa na uwezo wa kutambua mahitaji ya maswali katika mitihani ya ndani au ya kitaifa.
- (c) Walimu watumie mbinu shirikishi kama vile hadithi fupi, ngonjera, ushairi, igizo dhima na picha katika kufundisha umahiri wa *kuwa mstahimilivu na kuwa mwadilifu*. Watilie mkazo zaidi katika masuala yanayohusu uvumilivu, kufikia malengo, kuwa na mtazamo chanya, kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu, matendo ya uaminifu, usaliti, uwazi, wajibu na haki na haki za binadamu. Ufundishaji wa namna hii utawajengea wanafunzi kumbukumbu ya kudumu kuelewa kwa kina mahiri husika.

Ulingenifu wa Ufaulu kwa Watahiniwa kwa kila Umahiri katika Mtihani wa PSLE 2021 na Mtihani wa PSLE 2022

Na.	Umahiri	Mtihani wa 2021			Mtihani wa 2022		
		Ufaulu kwa kila Swalii		Wastani wa Ufaulu (%)	Maoni	Ufaulu kwa kila Swalii	
		Namba ya Swalii	(%) ya Ufaulu			Namba ya Swalii	(%) ya Ufaulu
1.	Kuithamini Jamii	2	82.4	62.9	Vizuri	9	55.43
		9	78.6			10	77.20
		10	44.3			12	73.38
		11	27.6			13	72.34
		13	38.7			14	51.37
		14	60.1			42	82.71
		20	84.8			-	-
		44	86.9			-	-
2.	Kuwa Mwajibikaji	5	21.6	60.8	Vizuri	15	68.68
		15	88.4			16	72.88
		16	58.8			17	74.85
		17	47.9			18	57.55
		18	72.0			20	24.91
		19	85.1			21	64.67
		21	42.8			43	86.80
		22	58.5			-	-

		28	46.5			-	-		
		33	78.1			-	-		
		42	69.3			-	-		
3.	Kuheshimu Jamii	1	35.2			1	87.70		
		3	5.6			2	21.76		
		4	60.9			3	43.83		
		6	75.9			4	69.35		
		7	44.8			5	74.86		
		8	76.9			6	42.79		
		12	49.1			7	18.34		
		32	33.1			8	84.76		
		41	37.9			11	56.14		
		43	81.1			19	36.95		
		-	-			22	20.31		
						41	88.40		
4.	Kuwa Mwadilifu	29	38.7			30	55.26		
		30	48.6			31	66.35		
		31	51.0			32	56.13		
		34	46.7			33	46.10		
		-	-			35	64.59		
						44	14.29		
							-		
5.	Kudumisha Amani	35	33.1			34	22.37		
		36	50.1			36	46.04		
		37	43.9			37	70.90		
		38	62.9			38	62.75		
		39	46.9			39	38.83		

		40	30.9			40	45.72		
		45	53.7			45	77.13		
6	Kuwa Mstahimilivu	23	7.1	41.2	Wastani	23	29..9 6	49.00	Wastani
		24	48.5			24	69.68 6		
		25	49.5			25	33.17		
		26	56.8			26	38.63		
		27	44.1			27	44.95		
						28	75.10		
						29	51.38		

